





**Ndege** Precision yashindwa kutua Uwanja wa Dodoma

UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
RC Mrindoko azindua operesheni kupanda miti Mil. 7.5 ifikapo Julai
Ilivyo vita vya serikali, hadi kupungua vifo vya vichanga
MPANGO WA MAENDELEO AFYA KITAIFA -MMAM
Samia aja na staili zake mpya kila mtu kufikishiwa huduma
Inaendelea Uk. 12

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Februari 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581223

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UTATA KIFO MFUGAJI

# Polisi: Amejinyonga mahabusu kwa kutumia nguo yake ya ndani

- **Ndugu** wagoma kuzika, waandamana kwa RC wakiwa na sababu tofauti... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### UJENZI BWAWA NYERERE WAFIKIA ASILIMIA 81



UTEKELEZAJI wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) umefikia...

## Serikali yaruhusu kuingiza mchele wa nje ya nchi kukabili makali ya mfumuko

UKURASA 4




Ndugu wa marehemu wakiwa nje ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi kabla ya kwenda kwa Kamanda wa Polisi wa mkoa huo. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**



Meghji Chana Ndumbaro Mchengerwa

## Sababu mawaziri kutodumu Wizara ya Utalii zatajwa

UK.2

**MICHEZO** **YANGA SC, FEI TOTO MAMBO MAZURI** UK.24 **KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Alliance for Africa Farmers Party (AAFP), Sudi Said Sudi, akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama Tandika, Dar es Salaam jana, alipokuwa akitoa ratiba ya mikutano ya hadhara ya chama hicho. Kulia ni Makamu Mwenyekiti Bara, Nancy Mrikaria. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Polisi: Amejinyonga mahabusu akitumia nguo yake ya ndani

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MFUGAJI aliyetambulika kwa jina la Samweli Bulunde, anadaiwa kufariki dunia baada ya kujinyonga kwa kutumia nguo yake ya ndani (kaptula) akiwa kwenye Kituo cha Polisi Kanoge, Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi.

Ni tukio linaoendana na upinzani wa hoja kutoka kwa familia ya marehemu, inayodai kuwapo maswali mengi yasiyo na majibu kuhusu alivyokamatwa, kifo chake kilivyotokea, kutokuwapo uthibitisho unaotolewa na mamlaka husika na kuhifadhiwa kituo cha polisi cha mbali na hapakuwapo taarifa zozote kwao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, akitoa ufafanuzi kuhusu kifo hicho jana, alidai kuwa mtuhumiwa alichukua uamuzi huo akiwa mikononi mwa polisi, akituhumiwa kuhusika na mauaji na kukodi watu kwa ajili ya kutekeleza mauaji.

Alidai kuwa baada ya mtuhumiwa kuhojiwa kuhusu tuhuma hizo, alikiri kutekeleza matukio matatu ya mauaji mwaka 2020 na 2022, pia kutoa Sh. 500,000 kwa ajili ya kukodi watu wa kutekeleza mauaji.

"Ni kweli tukio hilo lipo na limetokea ila tu inatakiwa mjue Jeshi la Polisi lina mbinu nyingi za kumkamata mtuhumiwa.

"Alikamatwa Febuari 5 na Febuari 6 alichukua uamuzi wa kujinyonga kwa kutumia mshipi wa kaptula yake ya ndani na alisema ndugu zake wasijue kama alikuwa ni mtu wa namna hiyo.

"Lakini kwa kuwa ndugu zake walikuja hapa na wakataka kujua, tuliwaambia na wao wakabaki wanashangaa, hawakuamini kama ndugu yao alikuwa na mambo hayo, tuliwaambia kama hawaamini amejinyonga, basi walete daktari wao aje apime mwili.

"Lakini mpaka sasa wameelewa na wamekubali kuchukua mwili kwenda kumzika ndugu yao mkoani Mwanza," alisema Kamanda Makame.

Kabla ya kuchukua mwili huo, ndugu wa marehemu walionyesha kutoridhishwa na chanzo cha kifo cha ndugu yao, hivyo walifunga safari mpaka kwenye Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi kujua kwa undani kilichomsibu ndugu yao.

Sama Kafalasa, msemaji wa familia hiyo, alidai: "Samweli Bulunde alikamatwa Febuari 5 mwaka huu eneo la Luhafye Tanganyika baada ya kupigiwa simu na Mwenyekiti wa Mtaa kuwa analalamikiwa na OCS (Mkuu wa Kituo cha Polisi) aliyefika pale.

"Yule mzee walishindwana na baadaye Mwenyekiti akataka apate taarifa ya kina kuhusu kukamatwa kwake.

"Basi OCS baada ya kutumia nguvu kumkamata, Mwenyekiti ilibidi awaachie ofisi lakini kweli mzee walimchukua na kumpeleka, siku iliyofuata tulijitahidi kufika kila kituo cha mkoa huu, hatukumpata hata kwenye rejista ya kipolisi.

"Baada ya siku kadhaa kupita huku tukiendelea kufuatilia, tuliambiwa mzee alijinyonga ndani ya kituo cha polisi.

"Sisi mnavyotuona hapa, wote ni familia moja, tumeona sasa tujiridhishe kwa Mkuu wa Mkoa, inawezekana alilifanya hilo maana na yeye ni mtu, na sisi tujiridhishe kwa madaktari wetu, hata kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa apimwe tuone kama hajaathiriwa na yule bwana ili nasi kama familia tukachukue mwili wa marehemu."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Luhafwe, Rafael Nkuba alisimulia kuwa Febuari 5 mwaka huu, majira ya saa 11 jioni, alipigiwa simu na familia ya marehemu akiwa pamoja na aliyefikwa na umauti, wakimjuza kuwa walikuwa ofisini kwake na alipofika aliwakuta watu watatu ambao ni mtoto wa marehemu, mjukuu wa marehemu na mzee wao ambaye baadaye alidaiwa kujinyonga kwenye mahabusu ya polisi.

Baada ya kufika walimweleza kuwa asubuhi wamepigiwa simu na askari polisi lakini kabla ya hapo askari huyo aliwahi kufika ofisini kwa mwenyekiti huyo akimlalamikia mzee huyo kuwa amemjibu maneno mabaya, hivyo amwite ofisini kwake waje wazungumze.

Hivyo, alimpigia simu akamwambia mzee huyo alikuwa amesafiri na akamjulisha askari huyo na baada ya mwezi mmoja kupita, ndipo walimpigia simu hiyo ya kuwa walikuwa ofisini kwake.

"Basi nilimpigia afande akaja, alikuja na askari mgambo wawili, mmoja ninamtambua, mmoja simtambui kwenye kijiji changu kama mgambo. Basi, baada ya kufika pale, akatumia mamlaka, akasema 'mwenyekiti huyu ni mtuhumiwa wangu', nikashangaa 'amekuwa mtuhumiwa wako tena? Kivipi we si mlalamikaji? Lile tatizo ambalo ulikuja kumlalamikia yule mzee ueleze, wajumbe wapo tutawashauri yaishe'.

"Akasema 'mimi tayari nimeshapiga simu mkoani wanakuja kumchukua, basi nikaona mimi sina haja sasa ya kuwasikiliza maana hii ni ofisi yangu, huwezi kumfunga pingu huyu mtuhumiwa bila mimi kujua kosa.

"Ninafikiri alimfunga kwa nguvu, mimi ikabidi niondoke, niache ofisi wazi. Baada ya hapo, askari wa mkoani (Mpanda) kweli walifika wakamchukua.

"Sasa mimi kama mwenyekiti sikujisikia, tunaonekana sisi wa mamlaka ya chini hatuna nguvu ya kuongoza na hatuna nguvu ya kumzuia askari kwamba hili usilifanye akakuelewa.

"Mimi siku ya tukio nilitoa taarifa kwa (Ofisa) Mtendaji Kata na kwa diwani kabla hawajaja kumchukua, nao walikuwa na taarifa," alisimulia mwenyekiti huyo.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa mtaa, Bulunde alikamatwa Febuari 5 mwaka huu na kudaiwa alijinyonga siku iliyofuata.

Alidai kuwa Febuari 13 mwaka huu, ndugu walifika kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambako hawakuonana naye, lakini wakapatiwa maelekezo ya kwenda kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa kupatiwa ufumbuzi.

Muda mfupi baadaye, Nipashe iliyokuwa na wanafamilia hao ilishuhudia wakikubaliana kutafuta daktari wao atakayetoa majibu ya chanzo cha kifo cha ndugu yao.

Hata hivyo, jioni ya siku hiyo mwandishi wetu alipowasiliana na wanafamilia hao, kabla ya kutekeleza walichokubaliana, wakawa na uamuzi mpya wa kuufuata mwili wa marehemu kwa ajili ya maandalizi ya mazishi.

Wanafamilia hao waliuchukua mwili wa marehemu hospitalini mjini Mpanda ulikokuwa umehifadhiwa Jumatatu iliyopita, na kuanza kuusafirisha kwenda mkoani Mwanza kwa ajili ya maziko baada ya kukamilisha shughuli za kuuaga.

# Sababu mawaziri kutodumu Wizara ya Utalii zatajwa

**Restuta James na Romana Mallya**

MABADILIKO ya viongozi yaliyodokezwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwaka jana, yamelikumba Baraza la Mawaziri baada ya juzi kuigusa moja ya wizara zinazotajwa kuwa ngumu, ya Maliasili na Utalii.

Jana Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza kwenye hafla ya kuapishwa viongozi walioteuliwa, aliwaeleza mawaziri hao waliobadilishana wizara kuwa wafahamu maadili serikalini, hivyo kwa wakati huu wabadilishane uzoefu na kuelezana changamoto ni zipi ndani ya wizara walizotoka.

Alimweleza Waziri Mohamed Mchengerwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ina historia kidogo na mafunzo mengi na imekuwa ni wizara iliyopata mawaziri wengi na ina mchango mkubwa wa fedha za kigeni pamoja na ajira.

"Bahati mbaya sekta hii ina vishawishi vingi, ninaamini Waziri (Pindi) Chana atakudokeza mengi aliyoona katika kipindi chake, ninadhani mjiepushe na vishawishi kama ni kwenye vitalu na mengineyo," alisema.

Kwa upande wa sekta ya utamaduni, Dk. Mpango alisema ndiyo inayokua kwa kasi hivi sasa na imekuwa ikiajiri vijana wengi na kumtaka akaitendee haki.

"Vijana wetu wanaitegemea hiyo sekta. Ukaimarishe ushirikiano kati yako na wasaidizi wako, watendaji bado tunaona changamoto katika wizara mbalimbali, ninaamini mtakwenda kuliangalia vizuri.

"Tumezungumza mara kadhaa, Mheshimiwa Rais ameeleza hii mivutano kati ya waziri, naibu waziri, waziri na katibu mkuu haina tija, mkae kama timu moja kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Watanzania katika sekta ambazo mmedhaminiwa kuziongoza. Mheshimiwa Rais hawa wote ni wazoefu, hakuna mpya, nilitamani nisisitize haya mnapoanza kazi," alisema.

### MABADILIKO

Juzi Rais Samia alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri kwa Mawaziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo Mchengerwa anabadilishana ofisi na mwenzake wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana.

Mabadiliko hayo yamewagusa pia Makatibu Wakuu ambapo Dk. Hassan Abbas ametolewa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda Maliasili na Utalii wakati Said Othman Yakub akipandishwa kurithi nafasi ya Dk. Abbas wizarani hapo akitokea Naibu Katibu Mkuu.

Kufuatia mabadiliko hayo, wachambuzi wa masuala ya siasa nchini wameiambia Nipashe kwamba huo ni mwendelezo wa kawaida wa kuisuka serikali ambao haukwepeki.

Aliyekuwa Mbunge wa Kahama (CCM), James Lembeli, alisema jambo la kuzingatia katika mabadiliko yanayogusa Wizara ya Maliasili na Utalii ni taasisi za wizara hiyo.

Alisema mabadiliko ya makatibu wakuu na mawaziri hayawezi kutatua matatizo yaliyoikabili wizara hiyo.

"Huko ndani ya taasisi hakuna kitu, kumeoza hilo ni tatizo moja kubwa. Kwa hiyo, hata Mchengerwa pamoja na uwezo wake alionao, utaniambia," alihadharisha.

Alisema waziri anayeteuliwa kuongoza wizara hiyo, anakabiliwa na changamoto ya kukosa taarifa sahihi za kufanya uamuzi wenye tija akieleza kuwa 'hakuna watu wa kumshauri vizuri.'

"Sana sana watamwingiza chaka... tatizo lingine hao wanaoingia hawaombi msaada kwa watu wanaoifahamu hii wizara na hata ukishauri, wanadhani unataka nafasi," alisema.

"Kuna watu ambao wana mapenzi mema na nchi, na ile wizara na wala hawataiji kulipwa... ngoja nikuulize, Mheshimiwa Rais alifanya kazi nzuri sana kuhusu The Royal Tour, sasa hivi unaisikia?" alihoji.

Alisema Taasisi iliyopaswa kubeba bango la The Royal Tour ni Bodi ya Utalii (TTB), ambayo alidai imekaa kimya.

### USULI NA HISTORIA

Wizara ya Maliasili na Utalii inatajwa kuwa Wizara 'isiyohimili mawimbi' pindi yanapotokea mabadiliko ya Baraza la Mawaziri.

Historia inaonyesha kuwa mwaka 2015 Hayati Rais Dk. John Magufuli alipokuwa akiingia madarakani, aliteua Naibu waziri bila waziri.

Katika miaka ya karibuni, Waziri aliyedumu kwa kipindi kirefu ni Dk. Hamis Kigwangala, ambaye alihudumu tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2020.

Taarifa zinaonyesha kwamba mrithi wake yaani Dk. Damas Ndumbaro, alihudumu kwa miaka miwili kuanzia mwaka 2020 hadi 2022 alipoingia Balozi Dk. Pindi.

Balozi Dk, Pindi anakuwa waziri pekee aliyedumu kwa muda mfupi zaidi kwenye wizara hiyo.

Jukumu zito linalomsubiri Waziri Mchengerwa ni kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), hususani ile ya mnada wa kielektroniki wa vitalu vya uwindaji.

# Waziri ashtukia jambo kubadili matumizi ardhi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula amepiga marufuku ubadilishaji matumizi katika halmashauri nchini usio na tija.

Dk. Mabula (pichani) alipiga marufuku hiyo juzi alipotembelea eneo lenye mgogoro lililokuwa shamba la NARCO Gezaulole, Kata ya Somangila, Manispaa ya Kigamboni.

Alisema kumekuwa na tabia ya kubadilisha matumizi kusiko na tija, akionya kuwa kunaharibu miji na mipango inayowekwa na halmashauri kupitia mipango kabambe licha ya kulipiga marufuku suala hilo mara kwa mara.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, ubadilishaji matumizi kwenye maeneo unafanywa na halmashauri husika na utaratibu wowote wa kubadilisha matumizi usiozingatia taratibu, unakwenda kinyume cha mipango miji sambamba na kuharibu miji.

Akitolea mfano wa Manispaa Kigamboni, Dk. Mabula alisema inao mpango kabambe ambao mipango yote katika halmashauri hiyo inatakiwa kuzingatiwa na kutekelezwa.

"Hapa mnao mpango kabambe unaotakiwa kutekelezwa na haujaanza katika utekelezaji lakini mnaanza kubadilisha matumizi maana yake katika uandaaji hamkuwa na uhakika mnapanga nini, hii haiwezekani," alionya.

Alitaka matumizi ya ardhi kwenye manispaa ya Kigamboni kubaki kama yalivyopangwa na kama kuna uhitaji wowote wa lazima, basi ni lazima ufahamike kama ni wa mamlaka au ni wa mtu binafsi.

Awali Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile alimweleza waziri huyo kuwa kwenye jimbo hilo kumekuwa na tabia ya ubadilishaji matumizi usio na tija alioueleza kuwa kwa kiasi kikubwa unachangiwa na baadhi ya watendaji wa sekta ya ardhi.



Dk. Mabula alitembelea eneo lililokuwa shamba la NAFCO Gezaulole Kata ya Somangila, Manispaa ya Kigamboni baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wa eneo hilo kwamba limeingia mgogoro.

# Raia wa kigeni mbaroni kwa tuhuma kufyatua noti bandia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU wawili raia wa nchi za Afrika Magharibi wamekamatwa mkoani Pwani kwa tuhuma za kuishi nchini kinyume cha sheria na kukutwa na karatasi za kuchapisha noti bandia.

Mjini Kibaha juzi, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge alisema raia hao walikamatwa Februari 10 mwaka huu kutokana na taarifa za raia wema, wakiwa wamejiandaa kuanza kufyatua noti hizo.

Aliwataja kuwa ni Livingson Ese Onayomake kutoka Nigeria na Bertrand Noubissie kutoka Cameroon ambao wote walikutwa eneo la Mapinga Wilaya ya Bagamoyo wakiwa kwenye nyumba ya New Era Nyembe anayedaiwa alikuwa mke wa Betrand.

Akielezea tukio hilo, Mkuu wa Mkoa alisema kuwa Februari 10 mwaka huu, timu ya maofisa uhamiaji ilifika eneo la tukio kufanya upekuzi na kubaini kuwa raia hao hawakuwa na hadhi ya kiuhamiaji.

Alisema katika upekuzi huo, Betrand alikutwa na karatasi zilizoandaliwa kwa ajili ya kuchapisha noti za fedha, kemikali na kasia (safe) la kutunzia fedha.

Vilevile, raia huyo wa Cameroon alikutwa na hati ya kusafiria yenye namba 0441270 iliyotolewa Yaounde Cameroon 12.04.2016 ambayo iliisha muda wake 12.04.2021 na aliingia nchini 02.11.2019 na viza aliyopewa iliisha muda wake 1.2.2020.

Livingson Ese Onayomake raia wa Nigeria alikutwa na hati za kusafiria 34 ambazo sio za kwake, ambapo kati ya hizo 32 ni za Nigeria na mbili ni za Ghana ambazo alidai alizichukua kwa lengo la kuwatafutia Visa Uturuki.

Livingson anadaiwa kuingia nchini 11.02.2020 na kupewa Visa ya matembezi ya siku 90 iliyoisha Mei 10, 2020 lakini aliendelea kuishi nchini kinyume cha sheria. Mtuhumiwa huyo raia wa Nigeria hakukutwa na hati ya kusafiria lakini alipoulizwa, alidai aliiweka rehani kwa Dayana wa hoteli ya King Sinza Afrika sana ili apate fedha za kujikimu.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Omary Hassan alisema Februari 9 mwaka huu, walipokea taarifa ya siri kutoka eneo la Mapinga na Februari 10 mwaka huu, maofisa uhamiaji waliwakamata watuhumiwa hao.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, uchunguzi wa tukio hilo umekamilika na hatua stahiki zitachukuliwa.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 51 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

SAID KUCHI MANYANYA

To:

Said Kuchi Manyanya
Plot No. 59, Block I,
Kisota Street, Mji Mwema Area
Kigamboni Municipality
**Dar Es Salaam Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 3rd day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

217282001



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 50 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

BAKARI MCHOME

To:

Bakari Mchome
Kifuru Street, Kinyerezi Area
Ilala Municipality
**Dar Es Salaam Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 3 day of march 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

217282001



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 46 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

HABSHI ABDALLAH HUSSEION

To:

Habshi Abdallah Hussein
Plot No. 897, Block B,
Ungindoni, Mji Mwema Street, Kigamboni Municipality
**Dar Es Salaam Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 03 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

217282001



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 61 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

JOAN NGAIZA

To:

Joan Ngaiza
Plot No. 29, Block B,
Mikocheni B Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

217282001

## MFUMUKO WA BEI

# Serikali yatoa kibali mchele wa nje ya nchi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeruhusu kuingizwa nchini tani 90,000 za mchele bila ushuru kama njia ya kupunguza mfumuko wa bei kwa nafaka hiyo.

Mchele huo utaagizwa mwezi huu na wafanyabiashara wa ndani ambao watapewa bei elekezi na serikali kuhakikisha bidhaa hiyo inauzwa kwa bei nafuu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mkakati wa kushusha bei ya bidhaa mbalimbali.

Alisema Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaendelea kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za mazao ya chakula na bidhaa muhimu nchini kwa lengo la kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mwenendo wa bei nchini.

"Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha wadau ikiwa ni pamoja na wazalishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali, watumiaji wa bidhaa hizo, wenye viwanda na wafanyabiashara kupata taarifa ili kufanya uamuzi utakaochangia kukuza uchumi na kipato katika ngazi ya mtu mmoja mmoja," alisema.

Waziri huyo alisema bei ya mchele kwa mwezi Februari ni kati ya Sh. 2,500 na 3,500 kwa kilo na kwamba haijabadilika kulinganishwa na bei ya mwezi Januari mwaka huu.

Alitaja mikoa yenye bei ya chini kuwa Iringa, Simiyu na Tabora na kwamba bei ya juu iko mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Manyara.

Kuhusu bei ya sukari, waziri huyo alisema kuna akiba ya sukari ya kutosha, hivyo wamekubaliana na wafanyabiashara kwamba hakuna haja ya kuagiza kutoka nje kwa kuwa itaharibu soko.

Alisema bei ya sukari kwa mwezi Februari ni kati ya Sh. 2,700 na 3,000 kwa kilo na kwamba bei hiyo imeonyesha uhimilivu kulinganishwa na mwezi Januari mwaka huu.

"Hali hiyo inatokana na jitihada zinazoendelea za kuvutia uwekezaji na kuongeza kiwango cha uzalishaji sukari nchini na bei ya chini iko katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Pwani na Singida na bei ya juu iko mikoa ya Ruvuma, Manyara na Lindi," alisema.

Akizungumzia unga wa ngano, waziri huyo alisema bei ya unga wa ngano kwa mwezi Februari ni kati ya Sh. 2,000 na 2,500 kwa kilo na imeshuka kulinganishwa na bei ya mwezi Januari mwaka huu ambayo ilikuwa Sh. 3,200 kwa kilo huku akibainisha kuwa bei ya chini iko maeneo mengi nchini na bei ya juu iko Mkoa wa Songwe.

Waziri huyo alibainisha kuwa bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti kwa mwezi Februari ni kati ya Sh. 4,750 na 7,800 kwa lita na ya mafuta ya kupikia ya mawese (Korie na Safi) ni kati ya Sh. 4,500 na 7,250 kwa lita.

"Bei ya mafuta ya kupikia imeonyesha uhimilivu kulinganishwa na mwezi Januari mwaka huu na bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti iko katika mikoa ya Manyara, Morogoro na Singida na bei ya juu iko mikoa ya Lindi, Pwani, Mtwara na Mara," alisema.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa nne kushoto), akikata utepe kama ishara ya kukabidhi nyumba kwa mshindi wa mashindano ya Qur- an, Abdulmariki Ramadhan (wa pili kushoto), katika eneo la Kigamboni, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto kwake ni Mwenyekiti Jumuiya ya Kuhifadhisha Qur'an, Sheikh Othman Kaporo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ndege Precision yashindwa kutua

**Na Elizabeth Zaya**

NDEGE PW 600 ya Shirika la Ndege la Precision jana ilishindwa kutua kwenye Uwanja wa Ndege Dodoma na kulazimika kurudi kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa mmoja wa abiria waliokuwa kwenye ndege hiyo aliyejitambulisha kwa jina la Joseph Samson, ndege hiyo ilikuwa inatoka Dar es Salaam kuelekea jijini Dodoma.

"Tupo hewani, nilikuwa nimekaa dirishani, wakati tunakaribia kushuka Dodoma nikaona injini imezima, rubani akatangaza kurudi Dar es Salaam kwa dharura kwa kutumia injini moja, ndege ikageuza kurudi, hali ilikuwa mbaya sana ndani ya ndege lakini tunamshukuru rubani kwa kutushusha salama.

"Ninaomba mamlaka husika zinazoshughulikia masuala ya anga kuhakikisha hizi ndege zinafanyiwa 'service' (ukarabati) ya kutosha kwani wanaweka rehani maisha ya watu wengi sana. Tunashukuru sana Mungu ametupigania kwani bila yeye mambo yangekuwa tofauti," alidai abiria huyo.

Meneja Masoko na Mawasiliano wa Shirika la Ndege la Precision, Hillary Mremi alithibitisha ndege yao kupata shida hiyo ya kushindwa kutua Dodoma.

Aliwatoa hofu wateja wao, akisema ndege zao ziko salama, akitamka: "Hizi ndege zimetengenezwa kwa injini mbili na endapo moja inapata changamoto, basi nyingine inaweza kufidia upungufu na kujiwezesha kutua salama.

"Marubani pia wamepitia mafunzo husika endapo kunatokea changamoto kama hii ili kutua kwa usalama.

## Watoto wenye ulemavu watelekezwa na wazazi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATOTO sita wenye ulemavu waliozaliwa na wasichana wenye umri wa chini ya miaka 20, wametelekezwa kwenye kituo cha kulea watoto wenye ulemavu wa akili na viungo cha Amani kilichoko Kata ya Chamwino, Manispaa ya Morogoro baada ya wazazi wao kushindwa kuwahudumia wakiwa kituoni huko.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Padri Beatus Sewando alibainisha hayo jana kwa waandishi wa habari, akisema kuwa wanne kati yao, walipelekwa mwaka 2021 na wawili mwaka jana na kituo kinaendelea kuwasimamia kimalezi.

Padri Sewando alisema watoto hao walifikishwa kituoni huko na mama zao wenye umri wa kati ya miaka 18 na 20 ambao hawajaolewa au wameacha shule kutoka maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Alisema wazazi hao walipofika kituoni huko kwa mara ya kwanza, walipohojiwa kuhusu kilichowasibu na kuzaa watoto katika umri mdogo, kwa nyakati tofauti kila mmoja alidai alijaribu kutoa mimba kwa njia zisizo za kitaalamu zikiwamo kumeza dawa ya kienyeji lakini mimba haikutoka na ndipo alipozaliwa mtoto mwenye ulemavu.

Padri huyo pia alitaja changamoto za watoto kuzaliwa wakiwa na ulemavu kuwa ni pamoja na mama kuchelewa kujifungua kwa kuzuia mtoto kutoka (kubana) kutokana na kuchelewa kufika hospitalini, hali ambayo husababisha kuzaa mtoto aliyechelewa kulia ambaye anapata matatizo kwenye ubongo.

Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani Morogoro, Jesca Kagunila alisema ni vyema mabinti hasa waliopo shuleni waepuke kujiingiza kwenye ngono zembe na hatarishi kwao kupata mimba kabla ya umri, kukomaza viungo vya uzazi na kusababisha kupata maradhi.

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 49 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

ZUBEIR ABDULLA

To:

Zubeir Abdulla
Plot No. 18, Block 39,
Sikukuu Street, Kariakoo Area
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 03 day of MARCH 2019 23 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 20 23

........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name........................................

Signature........................................

Qualification/Relationship

Date........................................

217282001

**HABARI KITAIFA**

# Daktari: Mgonjwa aliridhia kufanyiwa upasuaji wa tezi

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Bingwa wa Upasuaji Magonjwa ya Kifua, Shingo na Tumbo, Maurice Mavura (pichani) ameieleza mahakama kuwa Florence Samwel aliiridhia kufanyiwa upasuaji wa kuondoa tezi lake la upande wa kushoto na gharama za matibabu zilitoka kwenye bima yake ya NHIF.

Samwel alifungua kesi ya madai kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akidai fidia ya Sh. milioni 500 dhidi ya Hospitali ya TMJ, Hindu Mandal za jijini Dar es Salaam pamoja na Dk. Maurice Mavula kwa madai kuwa alifanyiwa upasuaji ambao utamfanya ameze dawa kwa maisha yake yote.

Daktari huyo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemarila wa mahakama hiyo wakati akitoa ushahidi wake dhidi ya kesi iliyofunguliwa na mdai kwa sababu yeye ndiye daktari aliyemfanyia upasuaji huo Florence ili apumue vizuri.

Akiongozwa na wakili wake, Ngassa Mboje, Dk. Mavura alidai mwaka 2018 alimfahamu Florence kutokana na tatizo alilokuwa nalo la tezi kushuka hadi eneo la kifua na kusababisha ashindwe kupumua vizuri, hivyo baada ya kuzunguka kwa madaktari wengi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) bila majibu, alielekezwa amwone yeye.

Dk. Mavura alidai June 27,2018 Florence alikwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili ambako alipofanyiwa uchunguzi kwa kupimwa vipimo mbalimbali, vilionyesha tatizo lake ambalo mtaalamu wa kushughulikia tatizo hilo alikuwa ni yeye.

Alidai kuwa Julai 7, 2018 alionana na Florence kwenye Hospitali ya Hindu Mandal, alimfanyia vipimo na alibaini alikuwa na tatizo kwenye njia ya hewa lililosababishwa na tezi ya kushoto kuvimba na kuelekea kifuani.

“Nilimweleza Florence tatizo lake na wakati tunazungumza alikubali kufanyiwa upasuaji kwa kuliondoa tezi hilo ili aweze kupumua vizuri kutokana na kwamba uvimbe huo ulisababisha yeye kutokupumua vizuri,” alidai Dk. Mavura.

Alidai kuwa tezi zipo mbili, lakini aliiondoa moja ya upande wa kushoto kwa sababu ndiyo iliyoonekana ina shida kutokana na vipimo alivyopimwa.

Baada ya Florence kuridhia upasuaji huo, Dk. Mavura alidai Julai 22, 2018, Florence alilazwa kwenye Hospitali ya Hindu Mandal kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji kwa sababu kabla ya upasuaji, lazima alazwe kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Alidai kuwa, siku hiyo mdai (Florence) alijaza fomu ya ridhaa kwa ajili ya kukubali kufanyiwa upasuaji huo kwa kutumia gharama za matibabu ya bima ya afya ya NHIF, alijaza fomu hizo za huduma hiyo ili aweze kupata huduma.

Dk. Mavura alidai Julai 23, 2018, alimfanyia upasuaji huo ambapo Florence aliendelea vizuri kwa siku mbili mfululizo, yaani Julai 24 na 25 na ilipofika Julai 26, 2018 aliruhusiwa kurudi nyumbani kutokana na maendeleo yake ya kiafya kuwa mazuri.

Hata hivyo, Dk. Mavura alidai kuwa ana uthibitisho (faili la magonjwa) kwa hayo yote aliyoyaeleza mbele ya mahakama kuwa mdai aliridhia kufanyiwa upasuaji kwenye Hospitali ya Hindul Mandal kwa kujaza fomu.

Alidai kuwa katika faili hilo la mgonjwa, kuna fomu ya gharama za matibabu ya bima ya afya ya NHIF na fomu ya ridhaa ya mgonjwa huyo kufanyiwa upasuaji na kuna fomu inaonyesha picha jinsi mgonjwa huyo alivyofanyiwa upasuaji.

Dk. Mavura aliiomba mahakama hiyo ipokee nyaraka hizo kama vielelezo, ambavyo Hakimu Rugemalira alivipokea na kutupilia mbali mapingamzi ya upande wa mdai.

Hakimu Rugemalira aliahirisha shauri hilo hadi Machi kwa ajili ya Dk. Mavura kumalizia kutoa ushahidi wake.

Florence ambaye ni mfanyakazi wa Wizara ya Kilimo, pia anataka alipwe Sh. milioni 53 kwa ajili ya gharama za dawa anazotumia kutokana na makosa hayo yaliyofanywa pamoja na gharama za usafiri wa kwenda kutibiwa Apollo.






Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. [48] OF [2023]

THE REPUBLIC

VERSUS

KASSIAN ANTONY NINDI

To:

Kassian Antony Nindi
Plot No. 1371, Block B,
Kisukuru Street, Tabata Area, Ilala Municipality
Dar Es Salaam Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the [03] day of [MARCH] 2019 [23] at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this [27] day of [01] 20[23]

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name..........

Signature..........

Qualification/Relationship

Date..........

217282001


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. [31] OF 20[23]

THE REPUBLIC

VERSUS

PROPERITY PRE & PRIMARY SCHOOL

To:
Managing Director
Prosperity Pre & Primary School
Temboni Street, Kimara B Area
Ubungo Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the [03] day of [MARCH] 20[23] at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this [27] day of [JAN] 20[23]

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name..........

Signature..........

Qualification/Relationship

Date..........

217282001


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. [28] OF 20[23]

THE REPUBLIC

VERSUS

RACHEL ERNEST MUSHI

To:

Rachel Ernest Mushi
Kulangwa, Goba Area
Ubungo Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the [03] day of [MARCH] 20[23] at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this [27] day of [01] 20[23]

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name..........

Signature..........

Qualification/Relationship

Date..........

217282001


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. [26] OF 20[23]

THE REPUBLIC

VERSUS

WAZIRI MUSTAFA NYONI

To:

Waziri Mustafa Nyoni
Plot No. 2707, Block C,
Goba Kunguru Area,
Ubungo Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the [03] day of [MARCH] 20[23] at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this [27] day of [JAN] 20[23]

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name..........

Signature..........

Qualification/Relationship

Date..........

217282001

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wateule Maliasili na Utalii jipangeni kwa historia mpya

**PANGUA** pangua ya Baraza la Mawaziri imekuwa haiachi kufanya mabadiliko kwa waziri na katibu mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Ni hali inayoonyesha ndani ya sekta hiyo kuna mambo mengi yanayokwamisha utendaji kazi na kuhitaji kutazamwa kwa jicho la pekee.

Ukiwatazama mawaziri waliowahi kuteuliwa kushika nafasi hizo, wengi waliishia kudumu kwa miaka mitatu na aliyehudumu kwa miaka tisa Zakhia Meghji, aliyeteuliwa katika zama za uongozi wa Hayati Rais Benjamini Mkapa, kati ya mwaka 1997 hadi 2005.

Aidha, Dk. Pindi Chana aliyeteuliwa Januari 8, mwaka huu amedumu mwezi mmoja na siku saba, akiweka historia ya waziri aliyechukua muda mfupi zaidi katika wizara hiyo. Hadi sasa katika awamu ya uongozi uliopo, awamu ya sasa, imekaa na idadi ya mawaziri watatu kushika washifa huo.

Hivi karibuni, Rais Dk. Samia alikemea baadhi ya watendaji wanaokwamisha wateule wake, kwa kuwa wanajua watakaobadilishwa na kuondolewa, ni wale walioteuliwa, jambo ambalo halikubaliki.

Baadhi ya wachambuzi wenye ubobevu kwenye fani ya hifadhi, wanasema bila ya kumulika watendaji wa wizara na taasisi zake, kuna uwezekano mkubwa mabadiliko kuendelea kuitikisa wizara hiyo kwa kipindi chote cha uongozi wa Rais Samia.

Mazingira kama hayo, Rais alishatamka pale alipozindua tume kufanya mapito katika taasisi za kiusalama nchini; Magereza, Polisi, Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (TAKUKURI), pia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Akizungumza kwenye hafla ya kuwaapisha mawaziri na makatibu wakuu wapya jana, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alisema viongozi wa juu wamechoka kusikia migogoro baina ya waziri na naibu, katibu mkuu na waziri na naibu na katibu mkuu wake, hali inayokwamisha utendaji.

Akamweleza mgeni Waziri Mchengerwa, kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ina historia kidogo na mafunzo mengi na imekuwa wizara iliyopata mawaziri wengi ikiwa na mkubwa wa fedha za kigeni pamoja na ajira.

Sekta hiyo ya utalii kwa ujumla, ina mchango mkubwa kwenye ukuaji uchumi wa nchi, hivyo ni muhimu kuifanya itulie, badala ya kulazimisha mabadiliko yanayojitokeza.

Tunaamini mabadiliko hayo yanafanyika kwa nia njema, kuboresha ufanisi kwa kadri Rais Samia anavyoona, nani atamfaa kwenye sekta gani katika kuwatumikia Watanzania na kufikia lengo tarajiwa.

Ni muhimu Mchengerwa na Katibu Mkuu wake, Dk. Abbas, wakajipanga kuisuka vyema wizara, kwa kuondoa makandokando yote, ikizingatiwa kuwapo raslimali zinazoingiza fedha nyingi kwa nchi.

Kote huko, ni taasisi zinazohusika na maliasili za nchi zinazoliingizia taifa mabilioni ya fedha kila mwaka, ni nyeti na muhimu kwa kuwa ndio zinatoa taswira ya nchi duniani kupitia utalii na ndiko kuna vitalu vya uwindaji vinavyosimamiwa na TAWA.

Watanzania wanahitaji uwajibikaji katika kazi kuhakikisha matokeo tarajiwa ya sekta ya utalii kutoa mchango wake kwa nchi linafikiwa, pamoja na kuondoa changamoto nyingi, ikiwamo kuongezeka kwa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori.

Upo uwezekano mkubwa wa mabadiliko haya kuathiri utekelezaji wa majukumu ya wizara kutokana na kwamba licha ya sheria kuwapo bado utashi wa kila kiongozi una nafasi kubwa kwenye kuongoza sekta, hivyo ni muhimu kuwapo uwajibikaji wa kutosha ili kupata matokeo chanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Suala la migogoro wafugaji na wakulima liangaliwe kwa kina

Na Halfani Chusi

**SUALA** la wafugaji na wakulima, kuuwana na kupeana majeraha limekuwa kitu cha kawaida, jambo ambalo kama halitafanyiwa utatuzi wenyetija linaweza kupelekea kutokea kwa maafa makubwa nchini.

Mara nyingi kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wakulima wakiwatuhumu wafugaji kwa kuingiza mifugo kwenye mashamba yao hali ambayo hupelekea kuzuka kwa mtafaruku mkubwa dhidi yao.

Inaporejewa, matukio ya kikatili miezi mitatu iliyopita huko Mkoani Pwani Wilaya ya Kibaha kulitokea tukio la kijana aliye shambuliwa hadi kuvunjwa mkono na wafugaji wa jamii ya kisukuma wakati alipokuwa akijaribu kuwazuia wasiingize mifugo kwenye shamba lake.

Hata hivyo, polisi mkoani humo ilichukua hatua ya kudhibiti ikiwa ni pamoja na kuwahamisha wafugaji waliokuwa karibu na mashamba ya wakulima.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo kupitia sakata hilo, akaagiza mtuhumiwa aliyetenda kosa hilo akamatwe na afikishwe kituo cha polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

"Kwenye kupambana na hali hiyo, tulishafika mpaka sehemu yenye migogoro, tukaamuru wafugaji waondoke eneo lile kwa sababu licha ya mifugo kuharibu mazao ya wakulima lakini bado ilikuwa inachangia kuharibu miundombinu na vyanzo vya maji" alisema.

Licha ya kuwapo kwa malalamiko hayo, bado kumeendelea kuripotiwa kwa matukio ya kinyama wanayofanyiana makundi hayo, hapo ndipo dhana ya kuwekeza nguvu kwenye utatuzi wa madhila hayo inapohitajika.

Mnamo Februari 2 mwaka huu, gazeti hili liliripoti wafugaji walivyouwa maofisa misitu kwa kutumia panga na shoka, kwenye msitu wa hifadhi ya kijiji cha Chakulu na Ilunde wilayani Uvinza, mkoani Kigoma.

Ni kitendo kilicholaaniwa vikali na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kupitia Mkurugenzi wake Ana Henga, akiitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhakikisha waliohusika na kutenda kosa hilo wanachukuliwa hatua za kisheria.

> **Mwaka jana niliikuta mifugo imetawala shamba langu ikabidi niwatafute wahusika lakini nilipowapata walikuwa wabishi kulipa mpaka kesi ilipofika mahakamani.**

Ni hali inayotishia amani kutokana na muendelezo wa matukio hayo, ambayo wafugaji wamekuwa wakiyafanya pale wanapohitaji sehemu za malisho kinguvu, ipo haja ya mamlaka husika kukaa chini na kutafakari kwa kina lini migogoro kati ya wafugaji na wakulima itafikia ukomo.

Kama imefikia hatua hadi askari anauliwa vipi kwa raia wa kawaida? Ni dhahiri kuna kitu hakipo sawa kati ya wafugaji na wakulima, jambo linalohitaji utatuzi wa kina.

Undani wa hilo kama Nipashe ilivyothubutu kudodosa, unaonyesha kuna wakati wafugaji wanakuwa wakorofi kwa wakulima, lakini wakati mwingine wakulima wanakuwa wakorofi kwa wafugaji. Hiyo mara huishia na sintofahamu kati ya sehemu ya malisho na kilimo.

Mkulima mwingine wa mahindi kijijini Msagali, katika wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, akasema mara nyingi hulazimika kulala shambani kulinda mifugo kama Ng'ombe na Mbuzi, isiingie shambani kula mazao.

"Ninalala shambani kwa sababu, nisipofanya hivyo wafugaji wanaweza kuingiza mifugo yao, nikakosa chochote kama ilivyokuwa mwaka jana.

"Mwaka jana niliikuta mifugo imetawala shamba langu ikabidi niwatafute wahusika lakini nilipowapata walikuwa wabishi kulipa mpaka kesi ilipofika mahakamani" Kibago anasimulia kilichomsibu.

Pia, mkulima wa mkoani Iringa, wilaya ya Kilolo, katika kata ya Nyanzwa, naye ana kilio sawa na mtangulizi wake, akiiomba serikali kuangalia namna ya kumaliza migogoro ya kila siku kati ya wafugaji na wakulima.

"Watu wanapigana, wanapeana ulemavu wa kudumu, wengine wanakufa kisa migogoro ya wafugaji na wakulima, hili si jambo la kufumbiwa macho, watu wanapoteza maisha" analalamika.

HABARI KITAIFA

# Serikali yapongeza mgodi ujenzi miradi ya kijamii

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Sera na Mipango Ofisi ya Rais - TAMISEMI, John Cheyo, ameupongeza Mgodi wa Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu ulioko Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga kwa utekelezaji wa miradi ya kijamii kwa ufanisi mkubwa kupitia fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR).

Amesema kuwa tayari miradi hiyo imeanza kuchochea kasi ya maendeleo kwenye maeneo hayo.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati ujumbe wa maofisa wa TAMISEMI ulipotembelea miradi ya afya na elimu iliyotekelezwa kupitia fedha za uwajibikaji kwa jamii zilizotolewa na mgodi huyo kwa Halmashauri za Wilaya za Msalala na Nyang'hwale mikoa ya Shinyanga na Geita.

Cheyo alisema amefurahi kuona miradi mbalimbali imekamilika na miundombinu ya elimu na afya imejengwa kwa viwango vya kuridhisha ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchochea kufanikisha mipango ya serikali ya kuleta maendeleo kwa wananchi hususani kwenye sekta za elimu na afya.

"Ninawapongeza Barrick Bulyanhulu na watendaji wa serikali kwa kusimamia ujenzi wa miradi hii na ninatoa wito kwa watumiaji wa majengo na vifaa vilivyonunuliwa hospitalini, kuvitunza ili vidumu na kuendelea kuhudumia wananchi wengi zaidi kwa muda mrefu," alisema.

Kaimu Meneja wa Uhusiano wa Jamii na Mazingira wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo, aliueleza ujumbe huo kutoka TAMISEMI kuwa miradi ikishapitishwa na halmashauri husika, mgodi unatoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha mradi sambamba na kufanya ufuatiliaji kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango na muda uliopangwa.

Baadhi ya miradi mikubwa ambayo ujumbe huo ulitembea ambayo imejengwa kwa fedha za CSR na Barrick Bulyanhulu ni sekondari ya Mwingiro, Shule ya Mchepuo wa Kingereza ya Kharumwa, ujenzi wa madarasa na kuboresha maabara kwenye shule za sekondari za Kayenze, Igalula, Busulwangili, Bugarama, Chuo cha VETA Bugarama, Chuo cha Wauguzi cha Ntobo na Kituo cha Afya Bugarama.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwingiro, Antony Fabian aliushukuru Mgodi wa Barrick Bulyanhulu na Serikali kwa kufanikisha miradi hiyo muhimu ambayo inaendelea kuboresha maisha ya wananchi.



Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BOT), Emmanuel Tutuba (wa pili kulia), akikabidhi zawadi kwa Gavana wa benki hiyo anayestaafu Prof. Florence Luoga, katika hafla iliyoandaliwa na Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa TBA, Theobald Sabi na Mkurugenzi Mtendaji wa TBA, Tuse Joune. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# DPP ashinda rufani, Mahakama Kuu ilikosea

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani imeondoa adhabu ya faini ya Sh. 71,519,800 badala yake imeamuru wajibu rufani, Papaa Olesikaladai na Batian Balee kutumikia kifungo cha miaka 20 jela baada ya kubaini Mahakama Kuu ilikosea.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu; Jaji Gerald Ndika, Jaji Mary Levira na Jaji Omary Othman Makungu wa mahakama hiyo Arusha baada ya kukubaliana na rufani iliyowasilishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kupinga hukumu.

DPP aliwasilisha rufani akipinga hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Arusha mbele ya Jaji Sirillius Matupa.

Wajibu rufani; Papaa Olesikaladai maarufu Lendemu na Batian Malee maarufu Peshuti walitiwa hatiani na kuhukumiwa kwa kosa la kukutwa na nyara za serikali na kupewa adhabu ya kulipa faini kila mmoja ya Sh. 71,519,800 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 20.

Wajibu rufani wanadaiwa kuwa Julai 29, 2017, kwenye Kijiji cha Ndarakwai wilayani Siha, Kilimanjaro, walikutwa na meno ya ndovu wawili yenye thamani ya Dola za Marekani 30,000 sawa na Sh. 67,260,000, mali ya serikali.

Inadaiwa shahidi wa pili, Ronald Lyimo na Joseph Masele waliweka mtego na kuwakamata wajibu rufani kwenye Kijiji cha Ndarakwai wakati wa ukaguzi walimkuta mjibu rufani wa kwanza akiwa na vipande viwili vya meno ya tembo na mjibu rufani wa pili alikutwa na kipande kimoja.

Inadaiwa vipande hivyo vilichukuliwa na kupelekwa kikosi cha kukabiliana na ujangili na kukabidhiwa kwa mtunza stoo, James Kugusa.

Mrufani alikuwa na sababu tatu za kupinga hukumu ya mahakama ya chini, anadai kwamba jaji alikosea kisheria kwa kwenda kinyume cha kanuni ambayo inaelekeza thamani ya nyara, kwa minajili ya kutoa hukumu alipaswa kutumia kifungu namba 87 kinachoelekeza utoaji wa adhabu kwa kesi hiyo.

Sababu ya pili, alidai mahakama ilikosea kisheria kwani hukumu ilitakiwa kutolewa kwa sheria ya Uhujumu Uchumi na sio Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

Sababu ya tatu anadai mahakama ilikosea kuwaamuru kulipa faini au kutumikia kifungo cha miaka 20.

Katika shauri hilo, mrufani aliwakilishwa na Wakili Penina Ngotea akisaidiana na Wakili Unice Makala.

Miongoni mwa hoja alizowasilisha mrufani anadai jaji wakati akitoa hukumu hakuzingatia hati iliyokuwa ikionyesha thamani halisi ya nyara.

Wajibu rufani hawakuwa na hoja ya kuwasilisha, waliomba mahakama iwaachie huru.


Mahakaman baada kusikiliza hoja za DPP, ilikubaliana nazo kwamba mahakama ya chini haikutakiwa kutoa hukumu kwa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori badala ya Sheria ya Uhujumu Uchumi.

"Mahakama inakubali kuwa wajibu rufani walipaswa kutiwa hatiani na kuhukumiwa kwa kosa la uhujumu uchumi chini ya kifungu 60(2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi.

"Kifungu hicho kinaelekeza kupewa adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela bila faini lakini mahakama ilitoa hukumu chini ya kifungu namba 86(2) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

"Mahakama inaona hoja hiyo ina mashiko katika rufani hii, rufani inakubaliwa, adhabu ya faini inaondolewa badala yake wajibu rufani watatumikia kifungo cha miaka 20 jela bila faini," lilisema jopo la majaji.

## KABWELA



# Zungu aipongeza benki kutoa madawati shuleni

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (pichani) ameipongeza Benki ya Stanbic kwa mkakati wake wa Stanbic Madawati Initiative unaolenga kutatua tatizo la uhaba wa madawati shuleni.

Kupitia mkakati huo benki hiyo imetoa msaada wa madawati 150 kwa shule mbili za sekondari za Gerezani na Dar es Salaam.

Katika hafla ya kukabidhi madawati hayo iliyofanyika Shule ya Sekondari Dar es Salaam juzi, Zungu alisema msaada huo unaendana na ajenda ya serikali ya kuboresha Sekta ya Elimu na mazingira ya kujifunzia kwa watoto, vijana na watu wazima kwenye taasisi zote za elimu.

Alisema mchango huo unaonyesha dhamira ya benki hiyo kusaidia sekta hiyo, akiwaomba wadau wengine wafuate nyayo zao.

"Huu ni mpango mzuri sana kwa sababu si tu kwamba benki inachangia madawati, bali pia inapanda miti nchi nzima kwenye kila shule inazozichangia.



"Hii italeta matokeo ya kudumu kwa kupunguza athari za mazingira zitokanazo na ukataji miti unaoathiri vibaya hali ya hewa. Mpango huu ni wenye faida na una sababu zote za kuigwa na wadau wengine," alisema Zungu.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga alisema msaada huo ni sehemu ya mpango unaoendelea wa Stanbic wa kusambaza madawati na miti shuleni nchi nzima ili kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi.

Aliongeza kuwa benki hiyo imejipanga kuboresha maisha kupitia programu zinazosaidia maendeleo endelevu ikiwamo elimu.

"Mwaka huu Mpango wa Stanbic Madawati unalenga kuchangia madawati 1,000 kwenye shule mbalimbali ili kukabiliana na uhaba wa madawati na kuwawekea wanafunzi mazingira mazuri ya kusomea," alisema Mtiga.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Dar es Salaam, Hossain Njau aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo, akibainisha kuwa umeondoa uhaba wa madawati shuleni huko.

Alisema sasa kila mwanafunzi atapata dawati na kiti kizuri, akiamini hali hiyo itaongeza ufaulu wao kwa kiwango kikubwa.

Uhaba wa madawati katika shule za msingi na sekondari nchini ni moja ya hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupitia ukaguzi wake kwa mwaka 2020/21.

Kwa mujibu wa CAG, hilo litawezekana ikiwa Hazina itatoa fedha za kutosha na kuweka mikakati inayotekelezeka ili kukabiliana na upungufu uliobainika.

Kupitia ripoti yake ya ukaguzi wa hesabu za serikali za mitaa, CAG Charles Kichere, ana angalizo lake akibainisha kuwa serikali haikufanyika kazi mapendekezo yake ya mwaka 2017 kuhusu kuwapo kwa tatizo hilo.

Machi 2017, CAG (kipindi hicho Prof. Mussa Assad) alitoa ripoti ya ukaguzi maalum wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini (za serikali na binafsi), akibainisha nyingi kuwa na hali mbaya ya uchakavu na uhaba wa miundombinu na samani.

CAG alipendekeza serikali iboreshe miundombinu iliyokuwapo na kujenga mipya huku akiwa na angalizo kwamba hali hiyo ingetokea pia sekondari kutokana na kasi ya ongezeko la wanafunzi ambayo ni ya wastani wa asilimia tano kila mwaka, iliyochagizwa na Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada, maarufu elimu bure.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Sumsung Afrika Mashariki, Tae Sun Lee (kulia), akifungua duka jipya la bidhaa za kampuni hiyo, Mlimani City, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo Tanzania, Manish Jangra na Meneja wa duka hilo, Said Kibao. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

## Ujenzi wa Bwawa Nyerere wafikia asilimia 81

**Na Maulid Mmbaga**

UTEKELEZAJI wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) umefikia asilimia 81.82 hadi mwishoni mwa Januari mwaka huu.

Mhandisi Mkazi, Lutengano Mwandambo, alibainisha hayo wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) iliyotembelea mradi huo ili kujionea maendeleo ya utekelezaji wake.

"Ujazaji maji unaendelea na sasa kina cha maji kimefikia mita za ujazo 131.02 kutoka usawa wa bahari," alisema Mwandambo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya DAWASA, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange, alisema lengo la ziara hiyo ni kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati akizindua ujazaji maji kwenye bwawa hilo.

"Rais Samia alituagiza sisi DAWASA tunufaike kupitia maji ya Mto Rufiji kwa kusambaza majisafi na salama kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani baada ya kuwa yamezalisha umeme," alisema Jenerali Mwamunyange.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alipongeza kazi nzuri iliyofanyika kwenye mradi huo huku akionyesha kufurahishwa na ushirikiano mkubwa uliopo kati yao na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

**Ujazaji maji unaendelea na sasa kina cha maji kimefikia mita za ujazo 131.02 kutoka usawa wa bahari.**

# 'Uelewa kuhusu elimu ya bima bado uko chini'

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mkuu wa Jubilee Allianz amesema uelewa kuhusu bima bado uko chini kwa wananchi wengi, akisisitiza kutolewa elimu zaidi kuhusu suala hilo.

Dipankar Acharya alitoa kauli hiyo wakati wa utoaji vyeti kwa mawakala zaidi ya 100 waliohitimu mafunzo ya bima yaliyotolewa na Benki ya NBC kwa kushirikiana na kampuni hiyo ya bima.

Mafunzo hayo yanatolewa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma za bima nchini.

"Nia yetu kama Jubilee Allianz na Benki ya NBC (wahitimu) mkawe mawakala wazuri sokoni, tunategemea makubwa sokoni. Bado ukuaji wa bima ni mdogo sokoni, ndiyo maana tumeona ipo haja ya kuwaingiza katika huduma hii ya kuuza bima," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mafunzo hayo yameyotolewa kwa mawakala hao ambao anaamini hawatapeleka taarifa ambazo siyo sahihi kuhusu bima.

Mkurugenzi Mkuu Msaidizi wa Kampuni ya Bima ya Jubilee Allianz, Abdul Suleiman alisema lengo ni kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa mawakala 6,000.

"Tumelenga kulikuza soko la bima nchini na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wake," alisema.

Kulifikia lengo hilo, Suleiman alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa mawakala wanaotoa huduma za bima ili watoe huduma bora kwa wateja na kutoa elimu kwa wale ambao hawana uelewa juu ya umuhimu wa kuwa nayo.

"Benki ya NBC na Jubilee Allianz tutaendelea kuwa bega kwa bega kuwapa msaada wa kitaalamu muda wote," alisema.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi Desemba mwaka jana, zaidi ya mawakala 100 wakipewa mafunzo ya bima kwa kipindi cha miezi sita.

"Leo hii asilimia 90 ya mawakala wa NBC waliofanya mtihani na kufaulu wanapatiwa vyeti ikiwa ni wiki chache zilizopita baada ya kupatiwa mafunzo ya uuzaji wa bima," alisema.

Januari 14 mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alibainisha kuwapo idadi ndogo ya Watanzania wanaonufaika na huduma ya bima ya afya.

Ummy alibainisha kuwa kati ya Watanzania takriban milioni 60 ni asilimia 15 tu wanapata huduma za afya mfumo wa kulipia kabla ya kuugua kwa kulipia bima ya afya.

"Kwa hiyo, katika kila Watanzania 100, ni 15 tu ndio wana bima ya afya na katika hao 15 ni Watanzania wanane tu ndio wana bima ya afya hizi kubwa za NHIF na bima binafsi -- NHIF asilimia nane, bima binafsi ni kama asilimia moja," Ummy alifafanua.



# SBL yatoa elimu athari unywaji pombe umri mdogo

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imeungana na wadau wa elimu mkoani Tanga, kutoa elimu ya kupambana na unywaji pombe kwa watu wenye umri mdogo hususani kwa wanafunzi.

Elimu hiyo inatolewa na SBL kwa kushirikiana na Ofisa Elimu Taaluma Sekondari wa Jiji la Tanga, Maurus Ndunguru na Ofisa Maendeleo wa Jiji la Tanga na Mratibu Mashirika ya Kijamii, Naetwa Kilango katika Shule ya Sekondari Nguvumali.

Kampeni hiyo iliyopewa jina la SMASHED, inalenga kupambana na unywaji wa pombe ya SBL, kwamba inatumia michezo ya kuigiza ya jukwaani.

Ofisa Elimu Taaluma Sekondari wa Jiji la Tanga, Maurus Ndunguru, alipongeza SBL kwa kampeni hiyo.

"Kampeni hii itasaidia sana vijana wetu wa shule, hasa katika shule hizi tano mlizozifikia, maana wanafunzi wamekuwa wakipata changamoto za ulevi. Nashauri pia, kampeni hii iweze pita katika shule zote mkoani Tanga," alisema Ndunguru.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma wa SBL, John Wanyacha, alisema: "SMASHED inatoa mafunzo muhimu juu ya athari mbaya za unywaji pombe katika umri mdogo kwa vijana na jamii, kwa makusudi mazima ya kulinda ndoto na ustawi wa vijana, ili kuhakikisha wanafanikiwa katika jitihada zao".

Alisema mpango huo umetekelezwa nchi tangu Oktoba mwaka jana kwa awamu, kuanzia Dar es Salaam na kuhamia mkoani Tanga.

Alisema zaidi ya wanafunzi 15,000 wamefikiwa na mpango huo katika mikoa hiyo miwili.

Ofisa Maendeleo wa Jiji la Tanga na Mratibu Mashirika ya Kijamii, Naetwa Kilango, alifurahishwa na mbinu za kibunifu za utoaji elimu kwa vijana na kuwaomba wadau wengine kubuni miradi ya kulinda ndoto za wanafunzi.

"Asanteni SBL kwa ushirikiano wenu katika kuwaasa vijana hawa na kuwapa mbinu za kulinda kesho yao. Kwa kweli vitendo vya matumizi ya pombe katika umri mdogo ni lazima vipigwe vita na SMASHED ni jukwaa muhimu sana," alisema Kilango.

Mwanzilishi wa asasi ya kiraia ya vijana iitwayo Bridge for Change, Ocheck Msuva alisema SBL inawapa vijana nafasi ya kupanga kesho yao wakiwa na maarifa ya kutosha kufanya maamuzi makini.

Alisema kampeni hiyo imetekelezwa katika shule tano za sekondari jijini Tanga ambazo ni Nguvumali, Kihere, Toledo, Masechu na Mnyanjari sekondari.

Aliongeza kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zenye kundi la watu wenye umri mdogo wa wanaotumia pombe.

Alisema utafiti uliofanywa mwaka 2019 katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro ulibaini kuwapo kwa mwenendo wa matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15.

# Utalii wa faru weusi waongeza idadi ya watalii Mkomazi

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

KAMISHNA Msaidizi wa Uhifadhi wa Mkomazi, Emmanuel Moirana, amesema utalii wa faru weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, umeongeza idadi ya watalii kwa asilimia 100 kati ya mwaka wa fedha 2021/2022, ukilinganisha na mwaka uliopita.

Amesema ongezeko hilo la watalii limechangiwa na uhamasishaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya The Royal Tour.

Moraina alisema katika ongezeko la wageni hao wengi wanatoka nchi za Ujerumani, Ufaransa, Hispania na Marekani.

"Kwa kweli tunamshukuru sana Rais Samia, ambaye ndiye mwongoza utalii namba moja nchini. Filamu ya Royal Tour, ambayo imetusaidia sana kutangaza hifadhi zetu na vivutio vilivyoko," alisema.

**Mbali na mafanikio hayo, alisema hifadhi hiyo imewekeza pia zaidi ya Sh.milioni 765 katika miradi mbalimbali ya ujirani mwema.**

Pia alisema Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limewasaidia kuboresha miundombinu ya hifadhi hiyo na kuwezesha kupitika kiurahisi wakati wa masika na kiangazi. Kwa mujibu wa Moirana, maboresho mengine makubwa yaliofanyika katika uhifadhi wa faru weusi ni ujenzi wa uzio wenye kutumia nishati ya umeme wa kawaida na wa jua.

Moirana alisema uzio huo unasaidia kuwalinda wanyama hao kutoingiliana na wanyama wanaokula nyama na kuwa salama zaidi pamoja na kuonekana kiurahisi na karibu kwa watalii.

Mbali na mafanikio hayo, alisema hifadhi hiyo imewekeza pia zaidi ya Sh.milioni 765 katika miradi mbalimbali ya ujirani mwema.

Aliitaja miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabweni, madarasa, ofisi za walimu, choo na kituo cha polisi katika Kijiji cha Kalalani Wilaya ya Korogwe.

Alisema ujenzi wa miradi hiyo ambayo ni utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema kwa jamii zinazozunguka hifadhi hiyo, ipo katika hatua mbalimbali na itakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Moirana alisema: "Lengo la miradi hii kusaidia wananchi kupenda, kusaidia kulinda hifadhi na kuzuia ujangili."




Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Mzee wa Kanisa la KKKT Usharika wa Kwabada, marehemu Lukemele Lupituko Mlelwa, wakiupeleka katika kanisa hilo, kijiji cha Kwabada, wilayani Muheza, mkoani Tanga mapema wiki hii kwa ajili ya ibada, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika wilayani humo. Marehemu Mlelwa, ameacha watoto 18, wajukuu 90, vitukuu 80 na kilembwe kimoja. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Jenista awanyooshea kidole watumishi wasio na maadili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Jenista Mhagama, amewanyooshea kidole watumishi wasio na maadili katika maeneo ya mipakani ambao wanatuhumiwa kuharibu mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kutokana na tuhuma hizo, ameapa kufa na wanaotuhumiwa kufanya uharibifu huo wa mifumo kwa sababu ya maslahi binafsi na hivyo kusababisha mtandao kuwa chini ya kiwango.

Mhagama alielezwa jana kukasirishwa kwake na tuhuma juu ya uharibifu huo wa mifumo alipokwenda jijini Arusha, kufunga kikao kazi cha tatu cha mafunzo cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Kikao hicho kiliwajumuisha washiriki 1,600 kutoka idara mbalimbali za serikali.

"Natoa onyo kwa watumishi wasio waadilifu acheni ili serikali na wananchi wapate maendeleo na mawasiliano kwa wakati. Endapo eGA itasogeza huduma hizo kwa wananchi hadi vijijini, ni wazi kuwa watapata maendeleo na serikali itapata taarifa mbalimbali kwa wakati," alisema.

Kauli mbiu ya mwaka huu ya eGA ni 'Mifumo jumuishi ya TEHAMA kwa utoaji bora wa huduma za umma.'

Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndombi, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wakurugenzi, wakuu wa taasisi, makatibu tawala na watumishi wengine kutumia serikali mtandao ili kuiwezesha serikali kupata mapato mengi, ikiwamo kuachana na matumizi ya karatasi.



# Kicheko wananchi Ushetu wakijengewa hospitali mpya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameondokana na tatizo la kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama baada ya kujengewa hospitali.

Huduma zinazotolewa kwa sasa katika hospitali hiyo ni zile za wagonjwa wa nje, maabara na afya ya mama na mtoto na Aprili mwaka huu wanatarajia kuanza upasuaji ili kuondokana na gharama za kusafirisha watu kwenda Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Hospitali ya Manipaa ya Kahama inahudumia wajawazito wanaojifungua kati ya 40 hadi 60 kwa siku, huku asilimia kubwa ya watoto hao wazazi wao wanatoka katika Halmashauri ya Ushetu, Msalala, Shinyanga Vijijini, Kaliuwa, Uyuwi, Nzega, Kigoma na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Geita.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu namna ambavyo hospitali hiyo ilivyosaidia kuwaondolea adha wananchi hususani wajawazito kutotembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya huku baadhi yao wakijifungulia njiani.

**Tulipokea Sh. bilioni 1.5 za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, imekamilika baadhi ya majengo na sasa baadhi ya huduma zimeanza kutolewa ili kuwanusuru wananchi kutembea umbali mrefu...**

Alisema awali wananchi walilazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya kutoka Ushetu hadi Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

"Tulipokea Sh. bilioni 1.5 za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, imekamilika baadhi ya majengo na sasa baadhi ya huduma zimeanza kutolewa ili kuwanusuru wananchi kutembea umbali mrefu...tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kutupatia wauguzi 44 wa kuanzia," alisema Mihayo.

Mihayo alisema hospitali hiyo itakuwa pia inatoa huduma kwa wananchi wa wilaya jirani za Kaliuwa, Uyuwi, Nzega mkoani Tabora, Kigoma upande wa Magharibi na Geita upande wa Mashariki na itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Mmoja wa wagonjwa waliofika hospitali hiyo kupata huduma, Rosemary Joramu, aliishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma za afya karibu akisema awali walilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda Kituo cha Afya cha Bulungwa au Hospitali ya Manispaa ya Kahama na baadhi yao walijifungulia njiani.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Athumani Matindo, alikiri baadhi ya huduma kutolewa katika hospitali hiyo ikiwamo wagonjwa wa nje na kuwataka wananchi hususani wajawazito kufika na kupima ili waanze kliniki kuepukana na vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema mwaka ujao wa fedha watatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo ambayo hayajakamilika ikiwamo ujenzi wa uzio wa hospitali hiyo ili kudhibiti wizi wa dawa na vifaa tiba na wagonjwa kuwa katika hali ya usalama.



Katibu Msaidizi Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi, Gerald Mwaitebele (kushoto), akitoa mafunzo ya maadili ya viongozi wa umma kwa madiwani na wakuu wa divisheni na vitengo vya Manispaa ya Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Madiwani waiangukia serikali kuboresha huduma za afya

**Na Vitus Audax,** UKEREWE

BAADHI ya wananchi na madiwani wilayani Ukerewe mkoani Mwanza wameiomba serikali kuimarisha huduma za afya katika visiwa kwa kujenga zahanati ili kutokomeza vifo vya wajawazito na watoto vinavyotokana na kucheleweshwa kupata huduma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao wamesema mara kadhaa wanawake wamekuwa wakipata adha wakati wa kujifungua, huku wengine wakijifungua katika mitumbwi wakielekea katika zahanati.

Diwani wa Kata ya Kagunguli, George Mchechera, alisema Februari 11, mwaka huu katika kata yake kilitokea kifo cha mama mjamzito aliyefariki dunia usiku wa manane wakati akipelekwa kupatiwa huduma katika kisiwa jirani chenye zahanati.

Alisema katika kata yake kuna visiwa vinne ambavyo wanaishi watu na kati ya hivyo viwili pekee ndivyo vyenye huduma ya zahanati.

Akielezea mikakati ya halmashauri hiyo katika kukabiliana na mahitaji mbalimbali wilayani humo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, Joshua Manumbu, alisema tayari wamepitisha bajeti ya Sh. bilioni 4.4 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2022/2023 wametekeleza bajeti yao iliyopitishwa ya Sh. bilioni 3.9 kwa asilimia 40, huku wakitarajia kuikamilisha kwa asilimia 100 kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya afya visiwani humo.

Diwani wa Kata ya Busya, Dickson Chaundi, alisisitiza usimamizi mzuri wa miradi ya serikali pamoja na uadilifu katika ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha bajeti iliyopitishwa inafikiwa ili kuwasaidia wananchi waishio maeneo mbalimbali katika visiwa vya Ukerewe.

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko, akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo alimwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza pamoja na Wilaya kuhakikisha wanapitia upya utendaji kazi wa wahudumu wa afya katika visiwa vya Ukerewe wakati serikali ikiendelea na mipango ya kuongeza vituo vya afya na zahanati ili kila mwananchi apate huduma stahiki na kwa wakati.

# RC awaonya wakulima wanaotorosha tumbaku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKULIMA wa tumbaku wilayani Sikonge mkoani Tabora wametakiwa kujiepusha na vitendo vya utoroshaji au uuzaji wa zao hilo kinyume na utaratibu katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye msimu mpya wa masoko.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Batilda Burian, alipozungumza na viongozi wa vyama vya msingi, wataalamu na maofisa mbalimbali wa serikali.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeweka utaratibu mzuri ili kuhakikisha tumbaku yote itakayolimwa msimu huu inanunuliwa kwa bei nzuri iliyoelekezwa ili kumnufaisha mkulima.



Alisisitiza kuwa katika msimu huu kampuni kubwa za ndani na nje zimejitokeza kununua tumbaku yote itakayozalishwa na wakulima kupitia vyama vyao vya msingi, hivyo haina haja ya kwenda kuuza kimaficho.

"Ni marufuku kwa mkulima yeyote kutorosha au kwenda kuuza tumbaku yake nje ya utaratibu uliowekwa, atakayebainika kwenda kinyume atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Dk. Batilda aliwataka kuzingatia kanuni, taratibu na malekezo ya wataalamu ili kulima kwa tija na kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kubainisha kuwa mwaka jana pekee jumla ya kilo milioni 30 za tumbaku zilizalishwa na mwaka huu wamekisia kuzalisha kilo milioni 60.

Akiongea kwa niaba ya wakulima, Meneja wa Chama cha Msingi Tumaini, Kata ya Mole, Paul Maziku, alisema utoroshaji wa tumbaku huchangiwa na wanunuzi kuchelewesha malipo ya wakulima na kwamba wakiacha tabia hiyo hakuna atakayetorosha zao hilo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku (WETCU LTD), Hamza Kitunga, alisema serikali ina dhamira ya dhati ya kuboresha shughuli za wakulima na kumaliza matatizo yanayowakabili.

Alisisitiza kuwa mwaka huu hawatakubaliana na kampuni yoyote itakayokuja na hadithi ya zamani kutaka kununua tumbaku ya wakulima kwa mkopo na kubainisha wazi kuwa kila mnunuzi atalipa fedha taslimu.

Meneja wa WETCU, Samwel Jokeya, alisema katika kipindi cha miaka mitatu uzalishaji wa zao hilo umeendelea kuongezeka maradufu katika mkoa huo na hivyo kuwezesha wakulima kuendelea kunufaika.

Alibainisha kuwa athari za ulanguzi na utoroshaji wa zao hilo bado ni kubwa kutokana na baadhi ya wakulima kutokuwa waaminifu, hivyo kupelekea mapato mengi ya wakulima kupotea, alishauri kila mkulima kujiunga na chama cha msingi.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 16, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Ilivyo vita vya serikali, hadi kupungua vifo vya vichanga**



**RC Mrindoko azindua operesheni kupanda miti Mil. 7.5 ifikapo Julai**

Ukurasa 13

### MPANGO WA MAENDELEO AFYA KITAIFA –MMAM

# Samia aja na staili zake mpya kila mtu kufikishiwa huduma

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa Tanzania inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MAMM), ikihesabu miaka 15 na nusu tangu kuanza kwake mwaka 2008, sasa ikiwa katika uongozi awamu ya sita.

Hata hivyo, Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete. aliyekuwapo wakati huo, akaahirisha kwa mwaka mmoja utelezaji huo wa MMAM tangu kupitishwa kisheria na bunge mwaka 2017. Kwa sasa serikali awamu ya sita, iko chini ya awamu ya Rais wa kwanza mwanamke nchini, Dk. Samia Suluhu Hassan.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwajulia hali wagonjwa wanaopatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Manyara, iliyopo mjini Babati, Novemba mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

Wakati MMAM inaandaliwa, kukashuhudiwa na watafiti kuwapo mapengo mengi ya utendaji katika serikali kufanikisha sera ya afya kitaifa, kukiwapo angalizo la hali mbaya kwa umma katika huduma iliko, pia gharama za kuhimili mahitaji hayo.

"Licha ya kuwapo mtandao mzuri wa huduma za afya ya msingi, bado kuna ugumu wa kufikia kutokana na sababu nyingi. Katika baadhi ya maeneo, watu wanazifuata huduma hizo umbali zaidi ya kilomita 10, huku ikitakiwa iwe umbali usiozidi kilomita tano," linaeleza andiko la kuundwa kwa MMAM.

Ni mazingira yanayotajwa kwamba, hata watumishi waliokuwapo hospitalini idadi yao walikuwa chini ya asilimia 32 ya hitaji halisi, hali kama hiyo ikitawala kwenye maabara na vifaa vya kitabibu.

Malengo ya MMAM yalikuwa kuleta mabadiliko ya kiafya, huku kukishuhudiwa utekelezaji zaidi wa maboresho hayo, ikiwamo huduma ya bima ya afya, ingawaje inatajwa robo tatu ya wananchi hawajafikiwa hadi sasa.

Kwa sasa utawala chini ya Rais Dk. Samia, umeamua kufanya mapinduzi ya kuboresha zaidi huduma bima ya afya, iwafikie wengi na kinachoendelea sasa ni muswada husika uko jikoni kufikishwa bungeni, ukapate baraka ya utekelezaji.

Sura ya miundombinu ya MMAM umeandaliwa, unaanzia ngazi ya chini kimuundo; zahanati kwa kila kijiji na kata kuwa na kituo cha afya, wilaya inakuwa na hospitali yake, mkoa unakuwa na hospitali ya rufani.

Ngazi hiyo ya kimuundo inapanda kwa kanda kuwa na hospitali yake ya rufani na taifa, kunakuwapo Hospitali ya Taifa Muhimbili na tawi lake Mloganzila, zote zikiwapo Dar es Salaam.

**SAMIA NA MMAM**

Katika awamu sita za uongozi wa nchi, kila awamu kiongozi wa nchi amekuwa na vipaumbele na mbinu za kuleta maendeleo ya umma na taifa.

Katika utekelezaji wa MMAM awamu ya tatu, Rais Dk. Samia akielekea kufikia mwaka wa tatu madarakani, suala la utekelezaji wake umechukua sura kadhaa, ikiwamo kuipa uwezo bima ya afya na kusimamisha kasi ya ujenzi kuelekea kwenye kukamilisha mapengo, pia kutanua wigo wa mahitaji ya ajira.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - TAMISEMI) Dk. Festo Dugange, anasema katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Samia, kuna jumla ya hospitali mpya za wilaya 135 zilizojengwa kitaifa

Dk. Dugange anasema, Rais Dk. Samia katika uongozi wake, ameimarisha utoaji huduma za afya kitaifa, akiwezesha ujenzi wa zahanati na kukamilisha maboma ya zahanati zaidi ya 1,000, pia vituo vya afya 390 kwa nchi nzima.

Naibu Waziri huyo, ambaye pia ni mbunge wa Waging'ombe, katika hotuba yake ya miaka 46 ya kuzaliwa CCM mkoani kwake Njombe, anasema katika eneo hilo la afya hospitali ya mkoani kwake Njombe, anajigamba juhudi za Rais Dk. Samia, kuwatetea wananchi waliofuata huduma za mionzi na nyinginezo, kutoka mikoa mingine.

Kwa mujibu wa Dk. Dugange, Njombe ni kati ya mikoa 10 iliyopata shilingi bilioni tatu za kujenga shule mpya maalum za wasichana, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita, inayoendelea kujengwa mkoani hapo, ambayo pia ni nyenzo ya usalama kwa mabinti dhidi ya mikasa kama ya mimba.

Akiwa ziarani, baada ya kizindua na kutembelea hospitali hiyo ya Njombe iliyojengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 27, Agosti mwaka jana, Rais Dk. Samia akawaambia wafanyakazi wake:

"Chapeni kazi, matakwa yenu tunayafahamu, ikiwamo mahitaji ya vitendea kazi, tutakwenda kujitahidi kuyatimiza ili muweze kufanya kazi vizuri."

Akaendelea:"Tulitaka kufanya haya muda mrefu nyuma, kazi za serikali ni hatua kwa hatua, kipindi hiki tumeweza kufanya haya na tunafanya kwa nchi nzima."

**AUNGWA MKONO**

Katika utekelezaji wa kuunga mkono serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Dk. Samia, taasisi mbalimbali za umma na zisizo za

**Inaendelea Uk. 12**

MAZINGIRA

# Mvuvi asimulia wanavyopambana na mazingira tata ndani ya bahari

**Na Christina Mwakangale**

NI saa 7:30 mchana, Nipashe inakutana na sauti za 'wapigadege' wa kuuza samaki ama madalali, zikipishana na kuingiliana kwa sauti: "Hii 15,000 yote haya chukua pale 30,000 hapa 35,000 kabeba huyo mpatie, watu wawili wale wanataka 3,000 hiyo 4,000…"

"Haya mchele (samaki) huo chukua 30,000 hapa 45,000 mpatie huyo 50,000 kabeba yule 53,000 mpe…lete mzigo mwingine, tumalize…"

Ukifika eneo la soko la samaki Kunduchi, kwa usiye mwenyeji, sauti hizo zitakuchanganya na utajiuliza wauzaji na wanunuzi wanaelewana! Unapoingia kwenye eneo la ndani ya soko, unapita kwa makini, ukinyata, kuepuka utelezi.

Ni takribani wapigadebe watatu, wakiwa wamepanda juu ya baraza lililojengwa kwa saruji au unaweza kuita meza, kizimba ambacho huwapo kwenye masoko mengi nchini, lengo ni kwa ajili ya kupanga bidhaa mezani zinazouzwa.

Nipashe inakutana na hali tofauti katika soko la Kunduchi, matumizi ya meza hizo hubadilika kulingana na muda na mara nyingine huwa jukwaa, mpigadebe hupanda juu, akisimama ili aonekane na anaowapigia debe, yaani wanunuzi.

Mwandishi wa habari aliyedumu hapo kwa takribani saa tano, anashuhudia mengi, ikiwamo mazingira ya shughuli hizo sokoni hapo, kundi la kinamama wengi wenye vazi maarufu katika ukanda wa pwani, dera, wakiwa wamekaa ndoo zao za plastiki za ujazo tofauti, lita 10 na 20.

Baadhi yao wana chupa ndogo za plastiki zenye maji, si ya kunywa bali kwa shughuli maalum na dharura, iwapo akashika samaki ajisuuze mikono kuondokana na shombo yao.

Pembeni ya kinamama hao, kuna kijana aliyevalia fulana ya mikono wazi, ameshika fagio akifanya kazi ya kusukuma maji (waiper), anasukuma tope la maji kuelekea, ulikolalia mteremko wa maji.

Kinamama hao kazini wapatao 20, nao wamewazunguka wapigadebe hao waliopanda juu na kusimama juu ya meza ya 'vizimba' vya samaki, kila mmoja akisikiliza kwa makini kila bei inayotajwa, akiwa na uwezo nayo ananyoosha mkono juu, asipopata mpinzani, bahati yake, anachukua mzigo wa samaki.

Pembezoni mwa soko yaani ulipoishia ukuta wa jengo hilo, wapo vijana kadhaa maalum kwa ajili ya kuparua samaki. Wapo wanaofanyia shughuli hiyo mezani, au sakafuni, wakitanguliza kibao kidogo chini cha ukubwa wa inchi mbili.

"Mazingira bado, hapa uje siku mvua imenyesha au msimu wa mvua ilipochanganya Februari hadi Aprili, hapatamaniki, tope maji hakuna. Unakuwa na chupa ya plastiki zilizotupwa uchota maji baharini ili ukishauza samaki, ujisuuze," anatamka mmoja wa wavuvi, anayejitambulisha kwa jina moja Issa.

Kwa muda Nipashe, inakaa sokoni hapo inaanza mahojiano na wavuvi, ambao kwa majira hayo ni wanaofika na samaki kutoka baharini, baada ya safari ya saa tatu au sita baharini kutafuta kitoweo hicho chenye umaarufu kwa wakazi wa ukanda wa pwani.

Katika mahojiano na baadhi yao ambao walifika kwa awamu, hawakutaka kupoteza muda, pamoja na kukubali kuhojiwa na kuelezea shughuli zao mafanikio kiuchumi na changamoto wanazokumbana nazo.



Mvuvi Salam Mohamed, akizungumza na mwandishi wa makala hii, ufukweni mwa bahari, eneo lilipo soko la samaki Kunduchi, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

**WADAU WAFUNGUKA**

Salum Mohamed (25), mvuvi na mkazi wa Kunduchi asili yake ni kisiwani Pemba, Zanzibar ana simulizi kwamba. Na muda mrefu kwenye uvuvi, akisema wavuvi huhama kutoka fukwe au soko tofauti kulingana na maslahi.

"Nilihama Pemba kipato kilikuwa kidogo, unaweza upate samaki ila usipate fedha. Bei ilikuwa ya chini. Nilikuwa nauza kwa mafungu na fungu moja lina samaki watano au sita, hatupimi kwa kilo…

"Ukitoka baharini kuvua mvuvi kuna dalali unampatia, anauza, mvuvi hapati, mi kwa siku napata 20,000 au 30,000 inategemeana. Samaki maarufu kupatikana hapa (Kunduchi) ni kolekole, taa, changu.

Salum anaendelea kuelezea huku mavazi yake bado yakiwa na ubichi kutokana na maji ya baharini, anasema pamoja na kuchukua saa nne au tano baharini, ipo siku hata nyumbani kwake kitoweo cha samaki hukosekana kutokana na hali ya bahari.

"Kutokana na upepo wa bahari, au shwari, unaweza usipate kitu, ila ulipata pesa unaotumia mahitaji ya nyumbani tu. Ila pesa ninayopata huwezi kuiweka akiba. Utakuta mmeenda uvuvini wawili, au watatu mnagawa fedha mliyopata.

Anasema zana za uvuvi wanazotumia ni ngalawa anayoitegemea kwa asilimia 90 ikitembea kwa upepo na kadri na anavua kwa kwa kutega ndoano majini akikadiria kikapu kimoja au nusu humchumkua nusu kutwaa.

"Bahari yaani hapa tulipo ufukwe ulikuwa mbali, miaka mingi lakini, ila sasa umesogea. Sijui ni kwa nini? Tunapokuwa baharini, upepo ukiwa mdogo ujue hii chombo chako kitatumia saa nyingi kufika eneo lako, anaeleza.

Hali ya baharini, Salum anaifafanua kwamba, joto linaongezeka na ufukweni ni kawaida kukutana na taka aina tofauti hasa za plastiki za chupa za maji, juisi au kimiminika chochote.

"Mfano siku bahari ni shwari kabisa hakuna upepo, kwetu sisi wavuvi si shwari kwa sababu chombo changu kinaendeshwa na upepo, hapo itanipasa nipige makasia hadi nifike na safari itachukua saa tano badala ya tatu au nne.

"Lakini, iwapo chombo kimeungwa mashine (motor) tungeweza kupata zaidi sababu tungeenda mbali, samaki wengi wapo kina cha mbali ukivua jirani na ufukwe unapata kidogo. Ila mashine hizo pia zingetusaidia siku ambazo bahari ni shwari yaani hakuna upepo," anasema Salum.

"Mwandishi kwanza unatumia muda kunihoji, wavuvi tuna changamoto nyingi, ushuru boti inapoingia tu tunalipa, ila mazingira si mnayaona, kila siwezi kuzimaliza sina muda, nataka nikaswali," anasema Salum muda mfupi baada ya kukutana na mwandishi wa makala, akiwa katika unadhifu anakipunga upepo na wenzake ufukweni, kandoni ya ngalawa yake.

# Samia aja na staili zake mpya kila mtu kufikishiwa huduma

**INATOKA UK. 11**

umma, chini ya kivuli cha Sheria, hali kadhalika zikungwa mkono na Sera ya Ushirikiano wa Sekta Binafsi na Umma (PPP) zinaunga mkono serikali.

Katika hilo, mnamo Novemba mwaka jana, Benki ya NMB ikakabidhi vifaa tiba kwa zahanati ya Kikatiti, ikisema inaunga mkono mwamko wa ukamilishaji wa zahanati hiyo uliofanywa na Rais Dk. Samia aliyechangia shilingi milioni 10 za ukamilishaji wa zahanati, wakati aliposalimiana na wananchi wa Kikatiti, mnamo Oktoba 2021.

Meneja wa NMB, Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper, anasema wanaunga mkono utawala wa Rais Dk. Samia, akiwatakia wananchi maendeleo, kwa kuwapatia kitanda cha kinamama kujifungua, godoro, pia mzani wa kuwapima uzito wagonjwa na watoto wanaozaliwa, pia stendi za dripu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Zainabu Makwinya, anasema pia NMB imechangia ukamilishaji wa zahanati ya Kikatiti, ikiiunga mkono Shirika binafsi liitwalo Cross Talent Share International (CTSI) iliyochangia shilingi milioni 135.38.

Makwinya anasema, baada ya Rais Dk. Samia kuchangia shilingi milioni 10 za ukamilishaji ujenzi wa zahanati hiyo, iliongeza hamasa za kiwilaya, mbunge wake kupitia bajeti ya Mfuko wa Jimbo, akichangia shilingi milioni tano.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Jeremia Kishili, katika hilo anahitimisha kwa hoja ya kushukuru uhamasishaji sawa vitendo wa Rais Dk. Samia, akinena:

"Zahanati hii ilisimama takribani miaka tisa ikiwa boma, lakini Mheshimiwa Rais alipoweka mkono wake, hamasa imekuwa kubwa na wananchi watanufaika na huduma. " Nao wananchi wa kijiji cha Kikatiti, wakamshukuru Rais kuamsha ukamilishaji wa zahanati yao, wadau kuchangia, pia serikali:

"Tunamshukuru mheshimiwa Rais kwani vifaa hivi vitatumika katika utoaji huduma na kutuondolea kero kubwa na gharama za kupata huduma za afya katika umbali mrefu.

MAZINGIRA

# RC Mrindoko azindua operesheni kupanda miti Mil. 7.5 ifikapo Julai

## •Aanza kwa kusafisha Soko Kuu Mpanda

**Na Neema Hussein, Mpanda**

VIONGOZI wa serikali mkoa wa Katavi, wameanza maisha wakiwa na ajenda mahsusi ya kimazingira, kwamba 'miti ni uhai'. Pia wana tamko mahsusi kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakimuunga mkono kutunza mazingira kitaifa.

Hapo wanazindua harakati za kimazingira, kupitia Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko, anayewaongoza wananchi kufanya shughuli mbalimbali katika kampeni ya kupanda miti na usafi wa mazingira kwa jumla.

Ni hatua iliyofanyika kwa mkoa wote, pale Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mrindoko, akiwagawa wakuu wa wilaya kusimamia hatua hiyo katika wilaya zote za mkoa wa Katavi.

Siku ya kwanza, Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Jamila Yusuph, akauongoza umma husika, wananchi na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, wakipanda miti katika maeneo mbalimbali, ikiwamo shuleni na kwenye vyanzo vya maji.

Ni wakati huo, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, naye anawaongoza wananchi na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, kupanda miti katika maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Filberto Sanga, akamsindikiza Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko, wao wakingonja kuwaongoza wakazi wa Manispaa ya Mpanda kufanya usafi katika Soko Kuu la Mpanda.

Baada ya kazi ya usafi sokoni, umma ukahamia kuungana na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mrindoko, katika kazi rasmi ya kuzindua upandaji miti.

Ilikuwa siku yenye nakishi ya mazingira, wakipanda miti katika chanzo cha maji cha Bwawa la Milala, Mkuu wa Mkoa, akatoa maagizo baada ya kukamilika hatua hiyo.

"Miti hii sio kwamba tumekuja kupanda, halafu tunaiacha ijilee yenyewe, wananchi mliopanda kila mmoja amepanda mti wake na wengine mmeshirikiana na viongozi kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA).

"Miti hii yote lazima itunzwe, isimamiwe na kuhakikisha hakuna hata mmoja unaokufa. Miti yote ipone na ikue, ili ilete manufaa ya kutunza chanzo chetu cha maji wakati huohuo, iweze kuvuta mvua ili tuendelee kupata mvua pamoja na hewa safi," anaagiza Mrindoko.

"Suala jingine kwa wananchi ambao tumewapatia miti kwa ajili ya kwenda kupanda kwenye kaya zao, kila kaya inapaswa kupanda miti mitano na ninawaomba kila atakayepata mti, asiende kuuweka kichochoroni. Uchimbe shimo, upande na uutunze usiliwe na ng'ombe au mbuzi," anasema.

Pia, anaigiza MUWASA kuanzia kipindi kama sasa, kijipange kutimiza kuwa na miti milioni moja, hali itakayowahakikishia mazingira ya kuwapo miti na iwe endelevu kupandwa kwenye vyanzo vya maji na kuhudumiwa.

Lingine ni Mkuu wa Mkoa, anapiga marufuku shughuli zote za kibinadamu zinazofanywa pembezoni mwa chanzo cha maji, Bwawa la Milala, kama vile kulima, kufuga na kuvua samaki.

"Nimesema bwawa hili ni muhimu, ni chanzo cha maji na tutakilinda kwa kushirikiana na wananchi waliopo maeneo haya, ni marufuku kufanya shughuli hizo, kwa sababu shughuli hizo zinajaza mchanga kwenye bwawa na kusababisha kina cha maji kupungua," anasema.

Pia, anatumia fursa hiyo kutuliza wananchi kutokana na mgogoro unaoendelea kwa wananchi wanaoishi karibu na chanzo hicho, akifafanua:"Najua hapa kuna mgogoro ambao haujafika mwisho.

"Nataka niwape taarifa maana nasikia kuna radio mbao nyingi ambazo zinaeneza mambo mbalimbali kila mtu kwa namna anavyojisikia, amekula ugali wake ameshiba anaanza kuwapotosha wananchi wenzake.

"Leo tumekuja hapa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira kwa mkakati wetu wa 'Ng'arisha Katavi Tunza Mazingira' Kamati ya Mawaziri Nane ilifika hapa imechukua taarifa, ilizungumza na wananchi na wakawaacha wataalamu ambao walikaa zaidi ya siku 14 kufanya tathmini ya kina ya wananchi wote walio katika Bwawa la Milala na maeneo yanayozunguka bwawa hilo.

"Taarifa ile tumekwishawasilisha kwenye Baraza la Mawaziri na tunasubiri maelekezo kuhusu hatima ya eneo hili ni ipi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi niendelee kuwaomba msifanye mwendelezo wa ujenzi wa nyumba na vyoo," anasema Mkuu wa Mkoa.

Anafafanua: "Kwa sababu tunasubiri maelekezo ya Baraza la Mawaziri, tutakuja kuitisha mkutano na kuwaeleza hatima ya bwawa hili na wananchi wanaishi maeneo haya,"

### MPANDA NA MAMBO YAKE

Justine Wambali ni Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Mpanda (MUWASA), anasema bwawa hilo linatarajiwa kutatua kero ya maji kwa wananchi wa Manispaa ya Mpanda kwa asilimia 100 kupitia mradi wa 'miji 28.'

Anasema utainua uzalishaji maji lita kutoka 1,050,000 (milioni moja na elfu hamsini kwa siku) hadi lita 19,050,000 (milioni kumi na tisa na elfu hamsini); mahitaji ya maji kwa kata 15 za Manispaa ya Mpanda kila siku, ni zaidi ya lita milioni 15.

Ofisa Mhifadhi Mkuu wa Halmshauri ya Mpanda, Aloyce Kilemwa, anasema kuanzia Desemba mwaka jana, hadi sasa, kuna miti milioni 3.5 imeoteshwa na kupandwa mkoani Katavi, akiahidi kazi hiyo ni endelevu, matarajio ni kupandwa miti milioni 7.5 ifikapo Julai mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akishirikiana na mwananchi mkazi jirani na bwawa la Milala, kupanda mti ulioandaliwa kwa ajili yake.



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, katika picha ya pamoja na wananchi walioshiriki kupanda miti katika chanzo cha maji cha bwawa la Milala.
**PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

AFYA

# Ilivyo vita vya serikali, hadi kupungua vifo vya vichanga

**Na Yasmine Protace**

NADHARIA ya kiafya iliyo bayana, ni kwamba malezi bora ya watoto umri chini ya miaka mitano yanaposimamiwa vizuri, yanasaidia kuwalinda watoto dhidi ya madhara kiafya, pia kuwaepusha na vifo.

Inatajwa msingi wa malezi bora ya watoto, unajumuisha kuwafikisha kliniki na kuwapatia lishe bora. Hapo, serikali

imekuwa ikitoa elimu kwa jamii namna ya kuwalea watoto wadogo, sasa kukishuhudiwa matunda.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema mama mwenye mtoto anatakiwa kuwafuatilia kwa karibu watoto kimalezi na makuzi, hali inayosaidia kupunguza vifo kwao, hasa kwa walio na umri chini ya miaka mitano.

Serikali nayo imekuwa ikihamasisha kila mtoto anayezaliwa, apelekwe kliniki kwa utaratibu uliowekwa, ili apate matibabu sahihi, ikiwamo kinga za chanjo.



Baadhi ya wadau wa afya , katika mkutano unaozungumzia Ripoti ya Afya ya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano. **PICHA: YASMINE PPOTACE.**

Wizara ya Afya inasema, utafiti unaonyesha vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kitaifa, ikiwa ni zao la juhudi za kiserikali kufikia afya bora ya mama na mtoto.

Waziri Ummy, anasema kuna juhudi kubwa za kiserikali katika afya ya mama na mtoto, kuchangia kupungua vifo vya watoto walio na umri chini ya miaka mitano. Anaeleza kwamba tafiti zinaonyesha vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa mwaka 2022 vimefikia 43 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai, ikilinganishwa na 67 kwa watoto 1,000 kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Ni kauli ya waziri kwenye uzinduzi wa matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania wa Mwaka 2022, uliofanyika katika ofisi ya Taifa ya Takwimu jijini Dodoma.

"Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kabla ya kutimiza mwezi mmoja, vimepungua kutoka vifo 37 mwaka 1990 hadi vifo 18 mwaka 2021, kwa kila vizazi hai 1,000," anasema.

Anafafanua kuwa vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, navyo vimepungua kutoka 65 mwaka 1990 hadi 28 mwaka 2021 kwa kila vizazi hai 1,000. Kihesabu anaeleza imeshuka kwa asilimia 56.

"Hayo ni matokeo makubwa ya juhudi zinazofanywa na serikali katika utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, unaolenga kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano hadi vifo 40 katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai, ifikapo mwaka 2025/26,"anasema Waziri Ummy.

Rai ya waziri ni kwamba, matokeo hayo ni muhimu kitafiti na kwa serikali, huku akimsifu Rais Dk. Samia na wadau wa kiserikali wanaofuatilia na kutathmini malengo yaliyofikiwa katika mipango ya maendeleo kitaifa, kikanda na kimataifa kwa afya ya uzazi na mtoto.

Waziri anasema, kiwango cha udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano nchini, nacho kimeendelea kupungua kutoka asilimia 34 kwenye utafiti wa mwaka 2015/16, mpaka asilimia 30 kwa mwaka jana.

Hapo anaitaja mikoa inayoongoza kwa udumavu na kuiga juhudi zinazofanywa na mikoa mingine, kupunguza adha ya magonjwa hayo.

# Mateso ya ukeketaji, ubakaji, VVU Shinyanga

**Na Shaban Njia, SHINYANGA.**

SUALA la ukeketaji, mambukizi ya virusi vya Ukimwi na ubakaji, vinaonekana kuwa tatizo katika maeneo ya vijijini mkoa wa Shinyanga.

Pia, Ripoti ya Polisi nchini, inaonyesha kuwapo ongezeko la asilimia 25.95 ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na kinamama, katika mwaka 2020 kulipokuwapo mikasa 7388, kutoka 5,803 ya mwaka 2015.

Ili kupambana nayo mkoani Shinyannga, Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT) imekuwa ikishirikiana na Klabu ya Waan dishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga (SPC) kukabili madhila hayo.

Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omary, anasema wananchi wanakosa imani pale mtuhumiwa anapokamatwa na kufikishwa kituoni na baadae anaachiwa, ilhali hawatambui haki ya kisheria ilivyo katika mkasa huo.

Anasema, watendaji wa kata wana wajibu wa kutoa mrejesho kwa wananchi kuhusu mashauri mbalimbali yanayoendelea, wananchi ili kujua yamefikia hatua gani kupitia vikao na mikutano vyao.

Pia, anawasihi wazazi na walezi kuacha tabia kukutana na kumalizana kwa kulipanana ama kwa mifugo au fedha, kwani anayeumia ni mtoto aliyefanyiwa ukatili huo na sio wao, hali kadhalika ni kosa kisheria.

Mratibu wa Ukimwi wa Halmashauri hiyo, Happynes Misaeli, anasema ni mazingira yanayoendana na kushamiri maambukizi ya virusi vya ukimwi, huku nao wakichukua hatua ya kutoa elimu, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Rafiki-SDO.

Anataja makundi wanayoyafikia ni vijana wa umri miaka 15 hadi 24, kwamba wapo hatarini, hivyo wanapatiwa elimu ya kutumia kondomu, ujasiriamali na kuwaandaa kuwa baba na mama bora. Zaidi inafanyika katika maeneo ya mikusanyiko kama Mwakitolyo na Tinde, kunakoongoza kwa maambukizi hayo.

Lyamidati ni kati ya kata 26 za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ambazo zimeshamiri matukio ya ubakaji. Hapo,Veronica Nduta, Diwani wa kata ya Lyamidati, anakiri changamoto hiyo, akifafanua hatua wanazochukua.

Anataja mwananchi akifanyiwa ukatili, wanaripoti na watuhumiwa wengi wamekuwa wakitoweka, huku muathirika akibaki na maumivu moyoni.

Anasema, mikakati waliyo nayo ni kutenga eneo la kujengwa kituo cha polisi, pia zahanati wakiandaa wodi ya kinamama na watoto, ili kuwaondolea adha wajawazito kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za kiafya.

Ofisa Mtendaji Joyce Mahina, anawashauri wananchi kuondoa woga wa kutoa taarifa kwa ofisi yake, kwani inabaki siri baina ya ofisi na mtoa taarifa, wao wakichukua hatua kuripoti polisi katika kata jirani ya Mwakitolyo, kupata msaada zaidi, huku

wakiwapatia elimu na uwezo wa kujiamini watoa taarifa.

**KUTOKA KWA WANANCHI**

Anita Joramu, kutoka kijijini Ihungi kwenye halmashauri hiyo, anasema hawafahamu namna sahihi ya kutoa taarifa ya ukatili wanapofanyiwa ukatili, wakibaki nayo moyoni, ndicho kinatawala kwa familia nyingi.

"Matukio ya ubakaji yanapojitokeza wakati tunajiandaa kwenda kutoa taarifa kwa watendaji wetu, tunaoga kwanza na tunapofika tunaambiwa tumeharibu ushahidi," anasema.

Pia, anaeleza kuna wakati baba katika familia hufika hatua wameshachukua mahari ya binti tangu akiwa masomoni.

Chausiku Vumilia, anakiri hayo, akiongeza kuwa hawafahamu hata namna ya kuwasilisha ushahidi wa matukio ya ukatili kijinsia kwa vyombo vya sheria, ikwamo mahakamani, hivyo wanapotakiwa kutoa ushahidi, ama wanajificha au kutoroka, kwa sababu ya woga, hivyo anaomba kuwapo msaada kuwasimamia kisheria.

Mkazi Ramadhani Juma, anasema kukabiliana na matukio hayo ya ukatili huo, kunastahili kuendana na kupewa elimu ya ilivyo huduma za kisheria, kuanzia na kituo cha polisi.

Hangwa Anthony anasema, kukosekana kituo cha polisi pia ni sababu ya kukithiri matukio ya kikatili kwa wanawake na watoto, kwani kunakosekana kinga ya kisheria na inaishia kwa wenyeviti wa vitongoji na vijiji.

Anataja gharama, kupeleka malalamiko kwa dawati la jinsia kituo cha polisi, inatajwa usafiri wa gari ni Sh. 4,000 na pikipiki Sh.1, 000, huku vituo vingine inawagharimu kati ya Sh.4 ,000 na 30,000.

Mkazi mwingine, Dorice Lugina, anasimulia wamekuwa wakitelekezwa na waume zao baada ya kuivisha mazao shambani, kuuza, kupata fedha na kwenda kuoa wanawake wengine na wanashindwa kutoa taarifa kwa sababu vituo vya polisi wanavyotegemea viko mbali na makazi yao.

Kijiji hicho sasa kimepitisha azimio, kwa anayetaka kuoa au kuolewa ni sharti kupima virusi vya Ukimwi.

Ofisa kilimo kata katika eneo hilo, John Shilinde, anasema kila msimu wanaume baada ya mazao kukomaa, huyauza na kutelekeza familia walizokuwa nazo awali.





# 'Wadau mazingira ibueni ajenda, vipaumbele muhimu'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wataalamu na wadau wa mazingira nchini kutumia vyema fursa za mafunzo yanayotolewa na wadau wa maendeleo ili kuibua ajenda na vipaumbele muhimu vya miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Andrew Komba, aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga warsha ya wadau na wataalamu wa mazingira inayolenga kuainisha vipaumbele vya miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi inayosimamiwa na Mazingira ya Dunia (GEF)kwa niaba ya Katibu Mkuu wa ofisi hiyo.

Alisema serikali kupitia ofisi hiyo kwa kushirikiana na GEF imeandaa warsha hiyo kwa ajili ya kuwakutanisha wataalamu na wadau wa mazingira ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya GEF mzunguko wa nane ambao unatarajia kutekelezwa katika kipindi cha miaka minne ijayo.

"Warsha hii ilikuwa na malengo makuu mawili ambayo ni kuainisha vipengele vya miradi ya GEF mzunguko wa nane na pia kupeana ujuzi na maarifa ya pamoja katika namna ya kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekuwa ikiendesha mafunzo na warsha ili kuhakikisha kuwa wataalamu na wadau wa mazingira wanaongeza ujuzi na maarifa katika usimamizi wa miradi ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo.

Aliwahakikishia wadau wa maendeleo ikiwamo GEF kuwa serikali itaendelea kusimamia vyema miradi yote ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa malengo ya miradi yanafikiwa kwa wakati.

Mratibu wa Mfuko wa GEF Kanda ya Afrika, Dk. Ibrahima Sow, aliwashukuru wadau na wataalamu wa mazingira walioshiriki warsha hiyo kwa kuwasilisha na kutoa maoni na mapendekezo yatakayoisaidia utekelezaji wa miradi ya GEF- mzunguko wa nane.

Alieleza kuwa maeneo matatu ya utekelezaji wa mradi wa GEF- mzunguko wa nane yatajielekeza katika mradi wa usimamizi katika maziwa makuu na mabonde ya maji, fedha za kujenga uwezo kwa wataalamu wa miradi pamoja na usimamizi wa miradi katika nchi zinazoendelea.

**Warsha hii ilikuwa na malengo makuu mawili ambayo ni kuainisha vipengele vya miradi ya GEF mzunguko wa nane na pia kupeana ujuzi na maarifa ya pamoja...**

# TBA yapokea bil.54/- ujenzi nyumba za watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA) katika kipindi cha miezi 18, umepokea Sh. bilioni 54.2 kutoka serikalini kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za wakala huo kwa waandishi wa habari.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ule wa ujenzi wa nyumba 3,500 za watumishi wa umma katika eneo la Nzuguni Dodoma ambao uliwekwa jiwe la msingi na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango Novemba 30, mwaka jana.

"Serikali imeshatoa Sh. bilioni 15.5 kwa kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 150 ambao umefikia asilimia 81 na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 150 za awamu ya pili ukiwa umefikia asilimia tatu,"alisema Kondoro.

Alisema mradi mwingine uliotekelezwa kupitia kiasi hicho cha fedha ni wa ujenzi wa nyumba 20 za viongozi jijini Dodoma ambao umegharimu Sh. bilioni tisa.

**Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za ndani inajumuisha ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye uwezo wa kuchukua familia 12 katika eneo la Canadian Masaki ambalo limefikia asilimia 99 za utekelezaji kwa gharama ya Sh. bilioni 4.6.**

Aidha alisema mradi huo ulitekelezwa ili kukabiliana na uhaba wa nyumba za makazi ya viongozi uliojitokeza baada ya serikali kuhamishia makao yake makuu jijini Dodoma ambao umeshakamilika kwa asilimia 100.

"Ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma katika eneo la Magomeni Kota, awamu ya kwanza na ya pili kwa gharama ya Sh. bilioni 7.8, ujenzi wa jengo la ghorofa nane lenye uwezo wa kuchukua familia 16 tayari limeshakamilika kwa asilimia 99 na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la ghorofa nane umefikia asilimia 25," alisema.

Kondoro alisema mradi mwingine ni wa ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi wa umma katika eneo la Temeke Kota ambapo linajengwa jengo la ghorofa tisa linalochukua familia 144 na utekelezaji wake umefikia asilimia tisa na utagharimu Sh. bilioni 3.3.

Mradi mwingine ni umaliziaji wa ujenzi wa nyumba tano za majaji katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Mtwara, Kagera na Shinyanga, kwa gharama ya Sh. bilioni 2.4 na nyumba nne zimeshakamilika na kuanza kutumika.

"Ujenzi wa nyumba ya jaji Kagera unaendelea na umefika asilimia 30 ya utekelezaji na miradi mingine inayotekelezwa ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi jijini Dodoma, awamu ya kwanza na ya pili."

"Ukarabati wa nyumba 30 jijini Dar es Salaam, ukarabati wa nyumba 66 za iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA), pamoja na ukarabati wa nyumba katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA kutoka TAMISEMI," alisema.

Pia alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23, TBA imetekeleza miradi mbalimbali kwa fedha za ndani ambapo Sh. bilioni 8.6 zimetumika.

"Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za ndani inajumuisha ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye uwezo wa kuchukua familia 12 katika eneo la Canadian Masaki ambalo limefikia asilimia 99 za utekelezaji kwa gharama ya Sh. bilioni 4.6," alisema.

Alisema TBA pia imeanza ujenzi wa jengo la ghorofa saba kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma katika eneo la Ghana Kota jijini Mwanza ambalo lipo hatua ya uchimbaji wa msingi.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daud Kondoro (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu majukumu na mafanikio ya wakala huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAKUKURU yaokoa mil.290/- za miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) mkoani Dodoma imeokoa Sh.milioni 296.5 za miradi ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapo, Sosthenes Kibwengo, alisema fedha hizo ni za makusanyo kupitia mashine za POS ambapo watendaji wamekuwa wakikaa na fedha mkononi badala ya kuziwasilisha benki kama sheria inavyosema.

Alisema TAKUKURU imefuatilia miradi ya maendeleo 49 yenye thamani ya Sh. bilioni saba katika halmashauri za mkoani Dodoma na kubaini kuna mapungufu mbalimbali ambayo yanajitokeza ikiwamo wananchi kutokatiwa risiti za makusanyo ya fedha.

Kutokana na hilo Kibwengo alisema TAKUKURU itaendelea kufuatilia fedha za miradi ambazo zinatolewa na serikali ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Alieleza kuwa kuna mapungufu ya usimamizi wa miradi hiyo kitendo ambacho kinachangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa mali za serikali.

Hivyo, aliwataka watendaji kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanasimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Akizungumzia suala la rushwa katika taasisi mbalimbali alisema serikali za mitaa inaongoza kwa kuwa na asilimia 10, elimu asilimia tisa, ardhi asilimia tano, afya asilimia nne na sekta nyingine ni asilimia 10.

Alisisitiza kuwa wananchi kudai risiti ili kuhakikisha wanapunguza upotevu wa fedha za serikali.



# Ujenzi barabara ya njia nne wasainiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), imesaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya njia nne yenye urefu wa kilomita 32 kuanzia Nsalaga jijini Mbeya mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) kwa gharama ya Sh. bilioni 38.7.

Mkataba huo ulisainiwa jana katika eneo la Kabwe jijini Mbeya baina ya viongozi wa TANROADS na viongozi wa Kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. LTD (CHICO) ya nchini China ambayo ndiyo iliyoshinda zabuni na kushuhudiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, alisema barabara hiyo ni sehemu ya mradi wa upanuzi wa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) sehemu ya tatu ambayo ni Igawa-Tunduma yenye urefu wa kilomita 218.

**Barabara hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Mbeya ambao umekuwa ukikwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi.**

Alisema barabara hiyo imeharibika kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu pamoja na kuongezeka kwa magari ya mizigo ambayo yamekuwa yakibeba mizigo mizito.

Alisema kwa mara ya mwisho barabara hiyo ilifanyiwa ukarabati mwaka 1993 hali iliyofanya barabara hiyo inayoiunganisha Tanzania na mataifa mengine ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC).

"Zabuni za ujenzi wa barabara hii zilitangazwa Juni 7, 2022 na kufunguliwa Oktoba 20, 2022 ambapo jumla ya zabuni nane zilipokelewa na kufanyiwa tathmini kisha kampuni hii ya CHICO ilishinda," alisema Mhandisi Mativila.

Alisema kwa mujibu wa mkataba huo kazi ya ujenzi wa barabara hiyo itakamilika baada ya miaka miwili kuanzia sasa mpaka Februari mwaka 2025.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliipongeza serikali kwa kuanza kutekeleza mradi huo ambao wananchi wamekuwa wakiusubiri kwa muda mrefu bila mafanikio.

Alisema mbali na barabara hiyo kuwa na umuhimu kiuchumi kwa wananchi wa mikoa ya Mbeya na Songwe pia utasaidia kulipendezesha Jiji hilo kutokana na ramani kuonyesha kuwa zitawekwa taa katika maeneo mbalimbali.

Alisema barabara hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Mbeya ambao umekuwa ukikwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, aliomba kwenye utekelezaji wa mradi huo asilimia kubwa ya wafanyakazi watoke katika Mkoa wa Mbeya ili wanufaike zaidi.

Alisema mkoa huo kwa sasa una watu zaidi ya milioni 2.8 na hivyo nguvu kazi ni kubwa ambayo ikiajiriwa kwenye ujenzi wa barabara hiyo inaweza ikapunguza tatizo la ajira.

Hivyo, aliitaka Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuandaa mpango kazi wa kulipanga upya ili liendane na hadhi ya Jiji pamoja na ubora wa barabara inayojengwa.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Mbarawa, aliagiza maofisa wa TANROADS kusimamia ujenzi wa barabara hiyo kwa kuhakikisha inatekelezwa kwa thamani halisi ya fedha zilizotolewa na serikali.

Alisema mradi huo ni mkubwa na unatakiwa kusimamiwa vizuri ili ijengwe kwa viwango vya hali ya juu na kuifanya barabara hiyo idumu kwa muda mrefu ambao umeainishwa kwenye mkataba.

Vilevile alisema katika mkoa huo kuna barabara zingine ambazo ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali ikiwamo ya Katumbasongwe-Kasumulu-Ngana-Ileje (Km. 90.1), Katumba-Mbambo-Tukuyu (Km78).



Baadhi ya vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Mbeya, wakiwa wamembeba Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa anayewakilisha mkoa huo, Ndele Mwaselela, baada ya kushinda kwenye uchaguzi uliofanyika juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM Mbeya yapata Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimekamilisha uchaguzi wa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC).

Uchaguzi huo ulisitishwa awali kutokana na dosari zilizokuwa zimejitokeza awali ikiwamo tuhuma za rushwa kwa baadhi ya wagombea.

Uchaguzi huo ulifanyika juzi ambapo Mkurugenzi wa Shule za Patrick Missin ya jijini Dar es Salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela alishinda uchaguzi huo.

Wagombea wengine kwenye uchaguzi huo walikuwa ni aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Primohamed Mulla, Saul Mwaisenye, Christopher Uhagile na Agness Ngoma.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya , Mwalimu Shaibu Akwilombe, alisema wapigakura kwenye uchaguzi huo walikuwa 63 na hakuna kura yoyote iliyoharibika.

Alisema Mwaselela alipata kura 35, Mulla ambaye alishika nafasi ya pili akipata kura 29, Uhagire kura moja huku wagombea wengine wawili waliobaki wakiambulia kura sifuri kila mmoja.

"Kwa matokeo hayo namtangaza Ndele Mwaselela kuwa ndiye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama taifa akiuwakilisha Mkoa wa Mbeya," alisema Mwalimu Akwilombe.

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa mshindi kwenye uchaguzi huo, Mwaselela alisema atahakikisha anashirikiana na viongozi wenzake kukijenga chama ili kuhakikisha kinaendelea kupata ushindi kwenye chaguzi mbalimbali.

Aliwaomba wanachama wa chama hicho kuvunja makundi yote waliyokuwa nayo ili kukiimarisha chama kwa maelezo kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa kumpata kiongozi wa chama na siyo makundi yasiyokuwa na maana.

Kabla ya uchaguzi huo, aliyekuwa anashikilia nafasi hiyo ni Dk. Stephen Mwakajumilo ambaye alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho mkoa.

## Wanaoharibu miundombinu ya barabara kushughulikiwa kiasili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila mkoani Mbeya wamewaonya wananchi wanaohujumu miundombinu ya barabara mkoani humo wakieleza kuwa watawashughulikia kwa kutumia njia za asili.

Mkuu wa machifu Mkoa wa Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, alipiga mkwara huo juzi jijini Mbeya wakati wa utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka Nsalaga jijini Mbeya mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Mkataba huo wenye thamani ya Sh. bilioni 138 ulisainiwa kati ya Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na Kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. LTD (CHICO) na kushuhudiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.

Chifu Mwashinga aliiomba serikali kuwaachia viongozi hao baadhi ya makosa yanayofanyika kwenye jamii ili washughulike na wahusika kwa njia wanazozijua wao.

Alisema wakati wa ujenzi wa barabara hiyo ya njia nne, watashiriki kwenye ulinzi na kwamba yeyote atakayehujumu watamshughulikia ili iwe fundisho kwa watu wengine.

"Unaweza ukawa unaiba vifaa hivyo ukidhani unawaibia Wachina kumbe unaowaibia ni Watanzania wenzio, sasa kwenye huu mradi mmoja akajaribu aone atakachokutana nacho huko, wengi wataumia wakijaribu kuhujumu barabara hii," alisema Chifu Mwashinga.



# Serikali yapiga 'stop' uchimbaji mawe, vifusi eneo la Ubago

**Na Mwandishi Wetu,** Zanzibar

NAIBU Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaaban Ali Othman, amesitisha uchimbaji wa mawe na kifusi katika shimo liliopo eneo la Ubago kwa kutofuata taratibu zilizowekwa kisheria.

Alisema eneo hilo linafanywa kazi kinyume na utaratibu kutokana na kutokuwapo kwa vielelezo vinavyothibitisha kuruhusiwa kwa kazi hiyo.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kushtukiza ya kukagua mashimo ya kifusi yanayotumiwa bila ya kufuatwa sheria eneo la Ubago Wilaya ya Kati Unguja.

Naibu Waziri alisema uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka ni uhujumu wa mali za umma pia linarejesha nyuma jitihada za serikali.

**Athari za kimaumbile zinaweza kuwa kubwa zaidi miaka ya baadaye endapo wananchi wataendelea kuchimba kinyemela mashimo ya mchanga, mawe na kifusi.**

Aidha, alisema kuchimba kifusi, mawe au mchanga ni lazima kufuatwe utaratibu uliopo au mfumo ili kudhibiti mapato ya serikali pamoja na kuzuia athari mbaya zinazotokana na uchimbaji usiozingatia viwango.

Alisema sasa hivi zoezi hilo la uchimbaji linafanywa kupitia maombi maalum ya kimfumo wa mtandao na siyo kinyemela kama walivyofanya na kwamba kigezo cha kuwa mmiliki wa eneo siyo sababu ya kuchimba rasilimali bila ya ruhusa ya mamlaka husika.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi, alisema wananchi wengi wanakwepa kufuata utaratibu uliowekwa na serikali kwa kisingizio cha kuepuka usumbufu wa kukata vibali jambo ambalo siyo kweli.

Alisema wizara itaendelea kuwafuatilia wote wasiofuata utaratibu wa uchimbaji na watakaobainika adhabu kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao pamoja na kutaifishwa kwa mali zitakazokutwa katika eneo husika.

Alisema athari za kimaumbile zinaweza kuwa kubwa zaidi miaka ya baadaye endapo wananchi wataendelea kuchimba kinyemela mashimo ya mchanga, mawe na kifusi.



Mkurugenzi wa Bandari Zanzibar, Nahaat Mohammed Mahfoudh, akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara katika Bandari ya Malindi, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yaanza kupambana na walanguzi wa tiketi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, imesema inalifahamu kwa kina suala la ulanguzi wa tiketi, kwamba imeanza kuchukua hatua kupambana na tatizo hilo.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Nadil Abdul-Latif, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa viti maalumu, Aza Januari Joseph.

Naibu waziri huyo alisema miongoni mwa juhudi hizo ni kuzuia kusafiri kwa abiria aliyeuziwa tiketi ya ulanguzi ambapo tiketi yake haifanani jina na kitambulisho chake chochote.

Alisema kampuni zote za meli za abiria zimeelekezwa kutumia mfumo wa kielektroniki katika mfumo wa uuzaji wa tiketi na kuondosha uuzaji wa tiketi zilizoandikwa kwa mkono ambazo husababisha ulanguzi.

Alisema mamlaka inaendelea na jukumu la kutoa elimu kwa kutoa matangazo katika vyombo mbalimbali vya habari mara kwa mara yanayowataka wananchi kununua tiketi katika maeneo maalum na rasmi na siyo mikononi kwa walanguzi.

"Mamlaka inatoa leseni kwa ofisi za kuuzia tiketi kwa kuzitambua ofisi hizo pia mamlaka hufanya operesheni maalum kwa siku za abiria wengi kwa kukagua tiketi za ulanguzi katika Bandari za Unguja na Pemba pamoja na kusimamia wale wote wasiokua na tiketi halali kuzuiliwa kusafiri," alisema.

Aidha, alisema kwa hatua hizo mamlaka imeweza kuondoa tatizo hilo kwa kiasi kikubwa na aliwataka wananchi waendelee kununua tiketi katika ofisi zilizo rasmi ili kuondoa suala la ulaguzi.

Pia alitaja sababu inayosababisha kiwango cha fedha anayolipa abiria ikawa ni tofauti na ile inayosomeka katika tiketi ni kutokana na abiria kutonunua tiketi katika ofisi rasmi iliyosajiliwa ya uuzaji wa tiketi na badala yake kununua tiketi mikononi kwa walanguzi.

Alisema: "Mheshimiwa Spika, mamlaka inaendelea kuwaomba wananchi kuacha tabia ya kununua tiketi kwa walaguzi na badala yake wanunue tiketi katika maeneo rasmi yanayouza tiketi yaliyosajiliwa na mamlaka".

Alisema ni kosa kisheria muuzaji wa tiketi atakayemuuzia tiketi abiria yenye bei tofauti na iliyoandikwa katika tiketi ya kusafiria.

**Kampuni zote za meli za abiria zimeelekezwa kutumia mfumo wa kielektroniki katika mfumo wa uuzaji wa tiketi na kuondosha uuzaji wa tiketi zilizoandikwa kwa mkono ambazo husababisha ulanguzi.**

# Dk. Mwinyi asaini miswada minne kuwa sheria kamili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesaini miswada minne ya sheria na kuwa sheria kamili.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, alibainisha hayo wakati akitoa taarifa kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu sheria hizo katika mkutano wa 10 wa baraza hilo.

Alisema miswada hiyo ya sheria iliyosainiwa ni Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namba 9 ya Mwaka 2006 na kuweka masharti yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo mingine yanayohusiana na hayo.

Alisema pia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma Namba 1 ya Mwaka 2007 na mambo mingine yanayohusiana na hayo.

Alitaja mwingine ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.

Aidha, spika huyo aliutaja Muswada wa Kufuta Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Namba 7 ya Mwaka 1996 na kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuwa chombo kikuu cha kufanya tathmini na kukusanya mapato yaliyoainishwa ili kusimamia na kutekeleza sheria zinazosimamia mapato hayo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Alisema: "Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 92(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020; naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo niliyoitaja, sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi".

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.122 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GRACE JANETH MATEMBA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**SYLVIA FLORENCE KAAYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of April, 2023
Dated at DAR ES SALAAM this 13 day of February, 2023

Senior Resident Magistrate

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SWALEHE IBRAHIMU NG'UNGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S0675/0120** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MBUGWE SEKONDARI** mwaka **2019**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/62347/2023**.

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA NDOA Namba 03 YA MWAKA 2022**
**EVA MAVUCHE CHABAI……………..MDAI**
**DHIDI YA**
**GERALD ELIAS MADUHU……………..MDAIWA**
**KWA: GERALD ELIAS MADUHU – POPOTE ULIPO.**


Mahakama hii inakufahamisha kwamba mdai amefungua madai ya Talaka dhidi yako nakala yake inapatikana katika Mahakama hii. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 06/03/2023 saa 2:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.

Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kuwepo, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa leo hii na Mhuri wa Mahakama tarehe 08 mwezi 02 mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MWANZA

## KUPOTELEWA NA CHETI



**DORIS MAEDA** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha Degree of Master of Public Administration and Human Resource chenye Index Number **2860** kilichotolewa na Mzumbe University mwaka 2010 pamoja na Academic Transcript for Masters. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/48808/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.167 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SHUKRANI DANIEL MBOGONI**
**OF Miyuji ward within Dodoma City Council**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**EMMANUEL RICHARD BIYENGO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **07 Day of 03, 2023**
**Date at Dodoma this 14 day of 02, 2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.10 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LUCY ZABRON MHANGO**
**OF Mloda Area within Chamwino District in Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**GRACE ZABRON MHANGO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **16 Day of 2, 2023**
**Date at Dodoma this 6TH day of January, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GERALD NATHANIEL MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T766AGJ, CHASSIS NAMBA: YM850D86729** na **ENGINE NAMBA:2Y6718685.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa:
**ARU/ARU/RB/241973/2022**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 249 YA MWAKA 2022**
**SHABAN JUMA MANDE ……………………………………MDAI**
**VERSUS**
**SHAIBU SOZI SALUM ……………………………………MDAIWA 1**
**ABISAI PETER NGAJIRO …………………………………… MDAIWA 2**
**ALEXANDER LUPINDO …………………………………… MDAIWA 3**

**KWA:**
**SHAIBU SOZI SALUM**
**ABISAI PETER NGAJIRO**
**ALEXANDER LUPINDO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.03. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 ya mwezi wa FEBRUARI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NTUZO BASHARI MSUYA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA ISUZU YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 981 DNR.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI
**KAH/TR /RB/120/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KITAPELA INVESTMENT AND GENERAL SUP LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **SCANIA** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 376 DMZ.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI:
**KAH/TR /RB/120/2023.**

## TANGAZO KWA UMMA

**Kampuni ya Reco Engineering** Company Ltd iliyopo Chang'ombe Dar Es Salaam inawatangazia wateja binafsi na kampuni zilizoleta kazi zao kwetu na hawajaja kuzichukua kwa muda mrefu hata baada ya kukumbushwa kila mara bila mafanikio yoyote kwamba wanapaswa kuja kuchukua kazi zao ndani ya wiki moja kuanzia tarehe ya tangazo hili vinginevyo kampuni haitahusika na upotevu wa mali au uharibifu wowote utakaojitokeza baada tangazo hili.
Tafadhali zingatia ya kwamba wakati wa kuja kuchukua mali yako utapaswa kuja na fomu ya uthibitisho wa kuleta kazi kwetu sambamba na hilo gharama za utunzaji mali zitahusika.

## FANIKIWA MICROFINANCE LIMITED

Fanikiwa

**TANGAZO LA MNADA**

**Work Ethic Company Limited** na **Held Auctineer** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Gari jijini la Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Deodatus Boniface Chongolo | TOYOTA ALPHARD-T114DUX | 03.03.2023 |
| Mussa Mohamedi Mtulya | TOYOTA MARK X ZIO | 03.03.2023 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315(Work ethic) au 0677014355(Fanikiwa)**

**OFISI ZA MATANGAZO**

*Mikocheni Industial Area,*

*Po.Box 31042, Dar es Salaam.*

*Mobile: +255 - 745 700 710.*

*E-mail: advertise@guardian.co.tz*

*Website: www.ippmedia.com*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yawasisitiza NATO kuharakisha msaada

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imewasisitiza washirika wake kuharakisha msaada wa kijeshi wakati mawaziri wa ulinzi wa jumuiya ya NATO wakiendelea kukutana kwa siku ya pili, huku Russia ikijitamba kuvunja ngome za Ukraine mashariki.

Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema jana kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Telegram kuwa wanajeshi wa Ukraine walirudi nyuma kutokana na mashambulizi ya Russia kwenye mkoa wa Luhansk, ingawa haikutoa ufafanuzi wa madai hayo kuweza kuthibitishwa na vyanzo huru.

Ripoti hiyo ilisema wakati wa mashambulizi hayo, Waukraine walirudi nyuma umbali wa kilomita tatu kutoka maeneo waliyokuwa awali, na kuongeza kuwa hata mstari wa pili wenye ulinzi mkali ulishindwa kulizuwia jeshi la Russia.

Hata hivyo uongozi wa jeshi la Ukraine, haukuzungumzia changamoto zozote mkoani Luhansk katika maelezo yake ya jana, ukisema vikosi vya Ukraine vilizuwia mashambulizi katika maeneo zaidi ya makazi 20, ikiwemo Bakhmut na Vuhledar, ambao ni mji ulioko umbali wa kilomita 150 kusini magharibi mwa Bakhmut.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, alisema Russia ilikuwa inafanya haraka kufanikisha mambo mengi iwezekanavyo kupitia mashambulizi yake ya sasa, kabla ya Ukraine na washirika wake kukusanya tena nguvu.

"Ndiyo maana kasi ni muhimu kwa sasa, kasi ndiyo kila kitu katika kufanya maamuzi, kutekeleza maamuzi, uwasilishaji, mafunzo, kuokoa maisha na kurejesha usalama, na nawashukuru washirika wetu wanaotambua kwamba kasi ni muhimu," alisema Zelenskiy.

Inaelezwa kuwa Ukraine inatumia risasi na makombora kwa kasi kubwa zaidi kuliko mataifa ya magharibi yanavyoweza kuvitengeneza, na inasema inahitaji ndege za kivita na makombora ya masafa marefu kukabiliana na mashambulizi ya Russia na kurejesha maeneo iliyoyapoteza.

Marekani na jumuiya ya kujihami ya NATO wameahidi kwamba msaada wa magharibi hautasita mbele ya mashambulizi yajayo ya Russia, huku Waziri wa Ulinzi wa Marekani Lloyd Austin, akisema anatarajia Ukraine kuanzisha mashambulizi yake yenyewe katika msimu wa machipuko kurejesha maeneo yaliyotwaliwa na Russia.

Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani Boris Pistorius, alisema utoaji wa ndege za kivita kwa Ukraine utajadiliwa, lakini siyo suala kuu kwa sasa.

Waziri wa Ulinzi wa Uingereza Ben Wallace, alisema Uingereza inatoa mafunzo kwa Waukraine kupigana kwa njia ya kimagharibi na kutumia risasi kidogo zaidi kuliko ilivyo kwa njia ya kisovieti.

Russia ambayo inauita uvamizi wake kuwa operesheni maalumu ya kijeshi yenye lengo la kuondoa vitisho vya kiusalama, ilisema NATO imeonyesha uhasama wake kuelekea Russia kila siku, na ilikuwa inazidi kujihusisha zaidi na zaidi kwenye mzozo nchini Ukraine.

***DW***



Ofisa wa uokoaji wa Jeshi la Polisi Afrika Kusini akiwatafuta watu waliopotea kwenye vifusi kutokana na mafuriko, jana. **PICHA: AFP.**

# Niger yapiga 'stop' mgodi unaomilikiwa na Canada

**AGADEZ, Niger**

MAHAKAMA nchini Niger imeamuru mgodi wa madini ya Uranium unaomilikiwa na kampuni ya Canada kaskazini mwa nchi hiyo kusitisha shughuli zake baada ya wanamazingira kuwasilisha kesi mahakamani.

Agizo hilo lilitolewa jana, huku Mahakama hiyo ya mjini Agadez, ikiamuru kusitishwa kwa shughuli za uchimbaji madini za kampuni ya SOMIDA, ambayo kwa kiasi kikubwa inamilikiwa na kampuni ya Canada ya Global Atomic, ambayo ilianza uchimbaji wa madini Novemba 2022.

Muungano wa mashirika ya kiraia mwezi Januari mwaka huu, uliomba Mahakama kuruhusu kuendeshwa tafiti mpya kuhusu athari za mazingira ukidai kuwa tafiti za awali hazikuwa sahihi na zilifanywa bila kushauriana vya kutosha na wakazi.

Niger ni moja ya vyanzo vikuu vya uranium duniani, madini ambayo yanatafutwa na mataifa duniani kote kama chanzo cha nishati ya nyuklia ambayo inaweza kupunguza kutegemea nishati ya mafuta. Inaelezwa kuwa hofu ya usalama na wasiwasi wa kimazingira juu ya utupaji wa taka zenye sumu ya nyuklia bado zipo, ikimaanisha kuwa nchi hiyo bado haijanufaika vya kutosha na uchimbaji wa madini hayo.

Aidha, inabainishwa kuwa Global Atomic inamiliki asilimia 80 ya mtaji katika kampuni ya SOMIDA, huku serikali ya Niger ikimiliki asilimia 20.

***VOA***

## 12 wafariki kwa mafuriko Afrika Kusini

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

TAKRIBANI watu 12 wamefariki katika mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa nchini Afrika Kusini, huku hali ya maafa ya kitaifa ikitangazwa, na kwamba kuongezeka kwa maji kunaathiri hasa mbuga ya watalii ya Kruger.

Mamlaka nchini humo ilisema jana kuwa hali mbaya ya hewa imesababisha athari katika majimbo manne kati ya tisa kwenye ukingo wa mashariki mwa nchi hiyo.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi nchini humo Lungi Mtshali, alisema jimbo la Mpumalanga kaskazini mashariki mwa nchi linaonekana kuathirika zaidi hadi sasa, pamoja na katika hifadhi ya Kruger.

Taasisi ya Kitaifa ya Utabiri wa Hali ya Hewa (SAWS), ilisema hifadhi hiyo ambayo ina ukubwa wa hekta milioni mbili, inapitiwa na mito kadhaa, ambayo mingi imekuwa na mafuriko tangu mwishoni mwa wiki iliyopita.

Msemaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (SanPark), Isaac Phaahla, alisema kutembelea mbuga hiyo kumezuiliwa kwa sababu baadhi ya barabara zimeharibika, lakini hali bado inadhibitiwa.

Mtabiri wa SAWS Puseletso Mofokeng, aliliambia shirika la habari la AFP, kwamba mvua zilianza kunyesha nchini humo wiki iliyopita, zikisababishwa na baridi kali ya ghafla katikati ya msimu wa joto, na kwamba zaidi ya milimita 200 za mvua zilinyesha kwa siku moja katika baadhi ya maeneo.

Pia Mofokeng, alitahadharisha kuwa mvua zaidi zinatarajiwa katika kipindi chote cha wiki kukiwa na hali mbaya ya joto, akiongeza kuwa maji ni mengi na hayawezi kufyonzwa na udongo hali inayosababisha mafuriko kutokea kwa urahisi zaidi.

Ofisi ya Rais ilitangaza hali ya maafa ya kitaifa mwanzoni mwa wiki, ikieleza kuwa serikali inapanga kutoa makazi ya muda, chakula na mablanketi kwa watu ambao wamepoteza makazi yao.

Aidha, pamoja na ukarabati wa gharama kubwa wa miundombinu nchini humo, uharibifu mkubwa tayari umeripotiwa huku barabara na madaraja yakiharibiwa pamoja na hospitali kuathirika.

Inaelezwa kuwa nchi hiyo ilikumbwa na mafuriko mabaya zaidi mwaka jana katika historia yake, na kwamba mvua kubwa ilisababisha maporomoko ya matope yaliyosomba kila kitu.

Pia inabainishwa kuwa hali mbaya ya hewa ilisababisha vifo vya zaidi ya watu 400 na wengi kukosekana, huku uharibifu ukiwa ni makumi ya mamilioni ya euro.

***RFI***

HABARI MICHEZO

# NYOTA YANGA WATAKIWA KUIMALIZA TP MAZEMBE

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa Yanga wamesema jukumu la kuhakikisha wanavunja mwiko wa kutopata ushindi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wanaposhiriki mashindano ya kimataifa pale watakapocheza dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), lipo kwa wachezaji wenyewe.

Mara ya mwisho Yanga kupata ushindi ilikuwa ni dhidi ya Zalan FC kutoka Sudan Kusini, katika mechi iliyochezwa Septemba 17, mwaka jana ikiwa ni hatua za awali za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wamewaeleza wachezaji wao wanachama na mashabiki wanahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo itakayochezwa Jumapili.

Kamwe alisema kuwapo kwa wachezaji raia wa DRC katika kikosi chao ni faida kubwa watapowakaribisha TP Mazembe katika mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Hili la Yanga kutofanya vyema kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hiyo ni sahihi kwa sababu takwimu zinaonyesha hivyo na wala si jambo la kubishania wala mawazo ya mtu. Ni kweli hatuna matokeo mazuri kwenye uwanja huo, siwezi kusimama hapa nikaanza kukanusha, na moja kati ya vitu ambavyo tumezungumza na wachezaji hilo lilikuwapo.

Hatukushinda nyumbani, tukafanya hamasa nyingine kubwa kuelekea kwenye mechi yetu dhidi ya Club Africain uliopigwa nyumbani, mwisho wa siku matokeo yake yalikuwa suluhu," alisema Kamwe.

Aliongeza wamewakumbusha wachezaji kupambana na kuhakikisha wanasaka matokeo mazuri kwa ajili ya kuwasahaulisha machungu wanachama na mashabiki wao.

"Hatuwezi kila siku tunafanya hamasa mitaani kukusanya watu, halafu watu wakija timu haipati matokeo mazuri, kwa hiyo safari hii ni jukumu la kuhakikisha tunavunja mwiko wa kutoshinda kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa," alisema Kamwe.

Alisema pamoja na ubora wa TP Mazembe, lakini wao wana wachezaji ambao wameshazoea kucheza na timu hiyo walipokuwa na AS Vita ambao ni Fiston Mayele, Djuma Shaaban, Yannick Bangala, Jesus Moloko na Tuisila Kisinda.

"Wachezaji wetu hawa walikuwa AS Vita Club na haikuwa mechi ya kawaida, walikuwa wakicheza na TP Mazembe mechi ya 'dabi', nyingine Kinshasa, halafu tena wanakwenda kucheza Lubumbashi, kwa hiyo wengi hawana ugeni sana kucheza dhidi ya timu hiyo. Hii haitotusaidia hapa tu, hata mechi ya ugenini," Kamwe aliongeza.



Daktari wa Kamisheni ya Ngumi, Hadija Khamis (kushoto), akimpima afya bondia, Karim Mandonga, katika zoezi la kupima afya mabondia watakaoshiriki mapambano ya ngumi ya Kili Boxing Toway yatakayofanyika Februari 25, mwaka huu Moshi, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mandonga aja na Kantangaze

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA maarufu nchini, Karim Mandonga ambaye anatarajia kupambana na Ally Bozinia kutoka Tanga amesema ataingia katika pambano hilo na kauli mbiu mpya iitwayo Kantangaze.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mandonga, alisema amejipanga vizuri kuelekea pambano hilo na anaamini ataendelea kuonyesha ushindani na kuwapa burudani mashabiki wake.

"Nitaonyesha maajabu siku hiyo, nataka kuonyesha mashabiki wangu mimi ni mtu kazi," alisema Mandonga.

Aliongeza anawataka mabondia wenzake kudumisha nidhamu na kujituma ili kufikia malengo yao ya kucheza katika viwango vya juu.

Wakati huo huo, zaidi ya mabondia 10 walijitokeza jijini jana kupima afya zao kwa ajili ya maandalizi ya kuelekea pambano la Kili Boxing litakalofanyika Februari 25, mwaka huu Moshi, mkoani Kilimanjaro. Mratibu wa Peaktime, Bakari Hatibu, alisema maandalizi ya pambano hilo yako katika hatua za mwisho na anawataka mashabiki wa ngumi kutoka sehemu mbalimbali kujitokeza kushuhudia mapambano yatakayochezwa siku hiyo.

"Kutakuwa na mapambano ya viwango vya hali ya juu siku hiyo, tunawaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuunga mkono mchezo huu," alisema Hatibu.

## Simba Queens yajivunia kikosi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amedai kitendo cha kubadilisha kikosi katika kila mechi kimemsaidia kufahamu uwezo wa kila mchezaji na sasa anaweza kupata matokeo mazuri kwenye michezo ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza.

Simba Queens iliibuka na ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Ceasiaa Queens, shukrani kwa Vivian Corazone aliyefunga magoli mawili pamoja na Aisha Juma na Asha Djafa. Katika mchezo wa juzi safu ya ulinzi ilikuwa na mabadiliko kidogo kwa kucheza Daniela Ngoyi, Fatuma Issa (Fetty Densa) safu ya ushambuliaji akicheza Asha Juma, mechi iliyopita na Baobab Queens walicheza Esther Mayala, Doto Evarist na Oppa Clement.

Lukula alisema kila mechi amekuwa akifanya mabadiliko ya kikosi kwa sababu anahitajika kutoa nafasi kwa kila mchezaji ili kuisaidia timu.

Kocha huyo alisema baada ya kumkosa mshambuliaji wao, Oppa Clement, alimpa nafasi Asha (Juma) ambaye naye alifanya vizuri majukumu yake.

## Ligi ya Mabingwa Mikoa Machi 10

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Mabingwa wa mikoa hatua ya makundi inatarajia kufanyika kuanzia Machi 10, mwaka huu katika vituo vinne ambavyo ni Kagera, Kigoma, Shinyanga na Katavi.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imesema michuano hiyo itachezwa kwa ligi ya mkondo mmoja na kila kituo kitakuwa na timu saba.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema katika taarifa hiyo kituo cha Kagera kitakuwa na timu za Buhaya FC ya Kagera, Shilabela FC (Geita), Mapinduzi FC (Mwanza), Nyamongo SC (Mara), Damali FC ( Simiyu), Nyumbu FC (Pwani) na Eagle FC ya Dar es Salaam.

Kituo cha Kigoma kitakuwa na wenyeji Aglo Sports Academy, Mambali Ushirikiano (Tabora), Singida Cluster (Singida), Arusha Ciry (Arusha), Tanesco FC (Kilimanjaro), Kiluvya FC (Dar es Salaam) na Kilosa United ya Morogoro.

Kundi C, ambalo litakipiga Shinyanga, litakuwa na wenyeji Maila Boys, Bus Stand (Dodoma), Aca Eagle (Manyara), Eagle Rangers (Tanga), Sharp Lion (Lindi), Mbuga FC (Mtwara) na Navy ya Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### ABRAHAM ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 25 ambaye anacheza AS Roma ya Italia. ***(Caught offside via Manchester Evening News)***

### CHELSEA YAMVAA BELLINGHAM

CHELSEA ipo tayari kujiunga katika kinyang'anyiro cha kumwania mchezaji wa kimataifa wa England anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 100, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund licha ya kutumia zaidi ya pauni milioni 600 katika madirisha mawili yaliyopita ya uhamisho. ***(Telegraph)***

### LEICESTER NA MADDISON

KLABU ya Leicester imeongeza kasi ya mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo, James Maddison mwenye umri wa miaka 26, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa England akikaribia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake wa sasa. ***(Telegraph)***

### FATI AGOMA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati, mwenye umri wa miaka 20, hana nia ya kuondoka Barcelona, licha ya ofa kutoka kwa Tottenham Hotspur, Arsenal na Bayern Munich, pamoja na Manchester United. ***(Mundo Deportivo)***

### BONO AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafuatilia uhamisho wa mlinda mlango wa Sevilla mwenye umri wa miaka 31 kutoka Morocco, Yassine Bounou, anayejulikana kama Bono, huku wakitafuta mbadala wa muda mrefu wa Mfaransa, Hugo Lloris, mwenye umri wa miaka 36. ***(AS)***

### MARTINEZ SOKONI ULAYA

ASTON Villa inatarajia kupata ofa kwa ajili ya mlinda mlango wa Argentina aliyeshinda Kombe la Dunia, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 30 msimu huu wa joto, lakini hawana shinikizo la kumuuza kwani mkataba wake unaendelea hadi mwaka 2027. ***(Mail)***

### QATAR YAIPANIA UNITED

AMIRI wa Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad al-Thani, anatarajiwa kutoa ofa ya zaidi pauni bilioni nne kwa Manchester United hadi kufikia Ijumaa hii. ***(Guardian)***

### ROQUE AGEUKA LULU

KLABU ya Athletico Paranaense imekataa ofa kutoka kwa Barcelona na timu nyingine mbili kwa ajili ya mshambuliaji wa Brazil, Vitor Roque, mwenye umri wa miaka 17 ambaye anaripotiwa kuwindwa na Arsenal. ***(Globo Esporte)***

### GUARDIOLA KUREJEA BARCA

BARCELONA itajaribu kumrejesha Pep Guardiola, pia kuwasajili, Rodri na Julian Alvarez kama Manchester City itapewa adhabu na Ligi Kuu England kwa kukiuka sheria za fedha. ***(Fichajes via Transfer News Live)***

### PORTER KUPEWA MUDA

CHELSEA haitampima kocha wake, Graham Porter, kwa matokeo ya muda mfupi, itampa muda na kumpima kwa matokeo ya jumla ya mpango wao wa miaka mitatu kwa timu wanayoitengeneza sasa. ***(The athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ATARAJIWA KUIBEBA PSG ULAYA

## ●●● Mshambuliaji huyo asema watasonga mbele katika michuano ya Ulaya lakini...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe alikuwa akitamani sana kuisaidia Paris Saint-Germain aliporejea kutoka katika hali ya majeruhi dhidi ya Bayern Munich, lakini bado ana uhakika wa kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbappe alikuwa na shaka kucheza mechi ya Jumanne ya hatua ya 16 bora wakati PSG ilipokuwa inaivaa Bayern Munich pale kwenye dimba la Parc des Princes.

Lakini mshambuliaji huyo aliyeshinda Kiatu cha Dhahabu cha Kombe la Dunia 2022 aliwekwa kwenye benchi na aliingia kipindi cha pili, muda mfupi baada ya Kingsley Coman kuifungia bao Bayern Munich katika mchezo huo.

Hilo ndio lilikuwa bao pekee na la ushindi kwenye mchezo huo ambao PSG ililala kwa goli 1-0 mbele ya Bayern, huku Mbappe akifunga mara mbili lakini yote yalikataliwa kwa madai ya kuotea.

Ingawa PSG sasa wamepoteza mechi tatu mfululizo katika mashindano yote ndani ya msimu mmoja kwa mara ya kwanza tangu 2011-12, Mbappe ana matumaini PSG itasonga mbele.

"Lazima tukumbuke mwisho," alisema Mbappe akiiambia Canal+.

"Tuna hasara, lakini tumeona tunaweza kuwaweka kwenye ugumu, tunaenda huko ili kufuzu.

"Ilikuwa haitabiriki, sikupaswa kucheza, lakini nilitaka kuwasaidia marafiki zangu. Tulifanya kazi nzuri.

"Wachezaji wetu wote wanatakiwa kuwa na afya bora kwa ajili ya mechi ya marudiano, kila mmoja anatakiwa kula vizuri na kulala vizuri."

Mbappe anapaswa kuwepo tangu mwanzo wa mechi ya marudiano ya Machi 8, mwaka huu na beki wa Bayern, Matthijs de Ligt aliiambia BT Sport: "Uliona katika dakika 30 zilizopita. Wakati Mbappe anaingia, timu ilikuwa tofauti.

"Lazima tuwe makini sana katika mechi ya marudiano."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,077,4

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE: SPURS KUPINDUA MATOKEO



**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte alisisitiza Tottenham Hotspur inaweza kurekebisha makosa yao yaliyotokea baada ya kufungwa bao 1-0 na AC Milan katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 Bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa Jumanne iliyopita.

Brahim Diaz alifunga bao la mapema dakika ya saba kwenye dimba la San Siro kwa kichwa kutoka eneo la karibu ya goli baada ya kipa, Fraser Forster, kuokoa shuti la Theo Hernandez.

Milan wangepata mabao mengi katika kipindi cha pili, lakini wakapoteza nafasi, na hivyo kuwapa Tottenham sababu za kuwa na matumaini kabla ya mechi ya marudiano ya Machi 8, mwaka huu jijini London.

Kocha wa zamani wa Inter, Conte anataka Uwanja wa Tottenham Hotspur ung'ae hali ile ile ambayo Spurs walipata huko San Siro, akiamini inaweza kusaidia kutinga robo fainali.

Aliiambia BT Sport: "Lazima ucheze michezo miwili. Ilikuwa hali nzuri sana. Naifahamu San Siro, na najua ugumu wa kucheza katika uwanja ule.

"Kwa hakika katika mchezo wa pili tunapaswa kucheza kwenye uwanja wetu na kwa hakika mashabiki wote watatengeneza mazingira mazuri ya kutusukuma kuwashinda Milan."

Spurs iliingia kwenye mchezo huo ikitoka kufungwa 4-1 na Leicester City kwenye Ligi ya England Jumamosi, na Conte hakuwa na Pierre-Emile Hojbjerg kutokana na kutumikia adhabu.

Pape Sarr na Oliver Skipp waliunganishwa katika safu ya kati, huku Yves Bissouma na Rodrigo Bentancur wakiwa nje kutokana na majeraha ya muda mrefu, na Conte alipenda alichokiona.

"Nadhani ilikuwa bora leo (juzi) - kiwango cha juu, na nadhani tulicheza dhidi ya timu nzuri. Usisahau Milan msimu uliopita ilishinda ligi nchini Italia," alisema Conte.

# De Jong atakiwa Barca

**BARCELONA, Hispania**

GOLIKIPA Marc-Andre ter Stegen anataka Frenkie de Jong kubakia Barcelona milele huku kiungo huyo wa kati Mholanzi akijiandaa kukabiliana na Manchester United, klabu ambayo ilijaribu sana kumsajili mwaka jana kwenye Ligi ya Europa, leo Alhamisi.

De Jong alikuwa mada ya mazungumzo kati ya Barca na United msimu uliopita wa joto na alianza msimu nje ya timu inayopendekezwa na Xavi Hernandez, lakini ameshinda nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza.

Na Ter Stegen amesema De Jong ni mfano bora wa kuigwa kwa vijana kama Pedri na Gavi.

"Analeta mengi kwenye timu," alisema Ter Stegen kuhusu De Jong, ambaye yuko katika msimu wake wa nne Barca.

"Nina maoni ya juu sana juu yake, lakini pia ninatarajia mengi kutoka kwake kwa sababu ana kipaji kikubwa.

"Nilitegemea angebaki kwa sababu, huyu ndiye aina ya mchezaji ninayemtaka katika timu yangu. Ni kweli, kulikuwa na uvumi na majadiliano mengi na chochote, lakini nina furaha tu kuwa hapa."



HABARI MICHEZO

# 33,324/-

# MKULIMA RUKWA ASHINDA SUPA JACKPOT MILIONI 248

Na Mwandishi Wetu




KAMPUNI ya Michezo, Burudani na Ubashiri SportPesa jana ilimtambulisha rasmi mbele ya waandishi wa habari mshindi wa Supa Jackpot ya mechi 13/13 Japhet Msangawale, mkazi wa Kijiji cha Sumbawanga, Rukwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, aliwashukuru waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari kwa kujitokeza kwa wigi katika hafla hiyo.

Tarimba alichukua wasaa huo pia kumpongeza Japhet Msangawale Mamboleo, Mkulima na mkazi wa Rukwa kwa ushindi huo wa Sh. milioni 248.6 ambaye, alishinda pesa hiyo siku ya Jumapili (Februari 12, 2023), saa tano usiku.

"Kama ilivyokuwa dhamira yetu tangu awali ya kuwawezesha Watanzania ambao wanabashiri na Kampuni yetu ya SportPesa, leo (jana) ninayo furaha ya dhati kumtambulisha na pia kumkabidhi mfano wa hundi ya pesa yake Japhet Msangawale Mamboleo ambayo ameshinda siku ya Jumapili usiku.

Mshindi huyu ni kijana mdogo wa miaka 25, ambaye kwa miaka takriban mitatu na zaidi alikuwa anajaribu kutimiza ndoto zake na leo hii, ndoto hiyo si ya kusadikika tena, bali imekuwa ndoto ya kweli, kwa yeye kushinda fedha hizi kupitia mchezo wa Supa Jackpot ambao mechi zake huchezwa siku za mwisho wa wiki."

"Ninyi ni mashahidi wetu ambao tumekuwa tukiwaalika mara kwa mara kutambulisha ama kuwapa taarifa juu ya washindi wetu wengi ambao wanashinda vitita tofauti tofauti vya pesa ikiwamo washindi wa Multibet bonus, Mid-week Jackpot bonus, Casino na yule wa milioni 147 wa bet spinner Peter Mbawala wa kule Dodoma, ambaye alishinda mwezi wa 12, 2022."

Akizungumza katika hafla hiyo ya kumtambulisha na kumkabidhi mfano wa hundi, mshindi wa Supa Jackpot ya mechi 13, Japhet ameishukuru SportPesa kwa ushindi wake na pia kama sehemu ambayo imewezesha yeye kushinda kiasi kikubwa cha fedha ambacho pengine isingekuwa rahisi kwake kukipata katika mazingira yake ya kawaida.

"Mwanzoni nilikuwa siamini kama nitaipata pesa hii, lakini, baada ya kushinda nilipata sms ya kunipongeza kwa ushindi wa Jackpot na baadaye usiku uleule nilipigiwa simu na mtoa huduma kwa wateja ambaye alinitaarifu juu ya ushindi wangu na kuniambia nitapigiwa simu ili nipewe utaratibu wa namna ya kuja Dar-es-Salaam, kuhakikiwa na kuthibitishwa na kisha kulipwa fedha zangu."

"Nimefarijika sana kwa namna SportPesa walivyokuwa karibu na mimi kimawasiliano tangu niliposhinda usiku ule wa Jumapili ya wiki iliyoisha. SportPesa wamenipa kila aina ya ushirikiano na kuhakikisha ninapata stahiki yangu kwa wakati."

Ikumbukwe tangu kuanzishwa kwake SportPesa imeshatoa washindi nane wa Jackpot na huyu Japhet anakuwa wa tisa na kila mshindi ni lazima alipe kodi, hata Japhet pia amelipa Sh. 24,867,179.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/02/23 | 18:00 | Blackpool vs Stoke City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 02. 18/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Birmingham City | 2.65 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 18/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Leeds United | 2.36 | 3.30 | 2.95 |
| 04. 18/02/23 | 18:00 | Hull City vs Preston North End | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 05. 18/02/23 | 18:30 | Portimonense SC vs Maritimo Madeira | 2.29 | 3.15 | 3.15 |
| 06. 18/02/23 | 20:00 | FC Winterthur vs FC Sion | 2.45 | 3.10 | 2.44 |
| 07. 18/02/23 | 20:30 | CD Leganes vs UD Las Palmas | 2.70 | 2.90 | 2.80 |
| 08. 18/02/23 | 20:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.27 | 3.45 | 2.95 |
| 09. 18/02/23 | 20:30 | RCD Mallorca vs Villarreal CF | 3.15 | 2.95 | 2.42 |
| 10. 18/02/23 | 20:45 | FC Groningen vs FC Emmen | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 11. 19/02/23 | 14:15 | SC Cambuur vs SC Heerenveen | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 19/02/23 | 15:00 | Motherwell FC vs Heart of Midlothian FC | 2.80 | 3.25 | 2.47 |
| 13. 19/02/23 | 16:00 | SD Huesca vs Granada CF | 3.30 | 2.95 | 2.34 |
| 14. 19/02/23 | 16:00 | Elche CF vs Espanyol Barcelona | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 15. 19/02/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Montpellier HSC | 2.50 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 19/02/23 | 18:15 | Rayo Vallecano vs Sevilla FC | 2.43 | 3.00 | 3.05 |
| 17. 19/02/23 | 18:30 | Santa Clara Azores vs FC Famalicao | 2.80 | 3.15 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 16/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 4024 | Bhayangkara Surabaya Utd vs Persija Jakarta | 3.32 | 3.27 | 2.03 |
| 11:10 | 5440 | Australia W vs Czech Republic W | 1.19 | 5.80 | 11.39 |
| 11:30 | 5047 | South Melbourne vs Moreland City FC | 1.23 | 5.58 | 9.30 |
| 13:00 | 1907 | Romania W vs Hungary W | 4.34 | 3.83 | 1.64 |
| 13:00 | 2244 | Pusamania Borneo vs PS Tni | 1.54 | 3.88 | 5.17 |
| 15:00 | 5700 | Rosario Central Reserve vs CA Lanus | 2.03 | 3.22 | 3.38 |
| 16:00 | 5298 | Ethiopian Medhin vs Adama City FC | 2.40 | 2.90 | 2.95 |
| 17:00 | 3330 | Udinese Youth vs Juventus Youth | 3.67 | 3.72 | 1.79 |
| 17:00 | 4201 | FC Goa vs Chennaiyin FC | 1.94 | 3.58 | 3.27 |
| 18:00 | 1229 | Coca Cola vs Haras EL Hodood | 1.58 | 3.63 | 5.97 |
| 18:00 | 1444 | Akwa United vs Gombe United FC | 1.63 | 3.38 | 5.20 |
| 18:00 | 4650 | Croatia W vs Finland W | 6.22 | 4.46 | 1.40 |
| 18:00 | 5271 | AL Adalh vs AL Tai | 2.92 | 3.72 | 2.18 |
| 18:30 | 3417 | SOL FC vs Denguele Sport | 2.83 | 2.63 | 2.73 |
| 19:00 | 2154 | Mazatlan FC U20 vs Pachuca U20 | 3.56 | 3.56 | 1.86 |
| 19:00 | 2745 | Dire Dawa Kenema FC vs Arba Minch Kenema | 2.42 | 2.97 | 2.86 |
| 19:00 | 3587 | Olympiakos Nicosia vs Anorthosis Famagusta | 3.68 | 3.26 | 1.92 |
| 20:00 | 2811 | Pyramids vs Enppi Club | 1.76 | 3.58 | 4.38 |
| 20:30 | 1373 | Sweden W vs China W | 1.28 | 4.96 | 8.47 |
| 20:30 | 1432 | Al-Ettifaq vs Al Ittihad Jeddah | 3.70 | 3.50 | 1.72 |
| 20:45 | 1381 | Barcelona vs Manchester Utd | 1.81 | 3.70 | 4.03 |
| 20:45 | 1865 | RB Salzburg vs Roma | 2.81 | 3.21 | 2.49 |
| 20:45 | 2237 | Shakhtar Donetsk vs Rennes | 3.21 | 3.31 | 2.19 |
| 20:45 | 2270 | Bodo Glimt vs Lech Poznan | 1.71 | 4.01 | 4.21 |
| 20:45 | 2441 | Sporting Braga vs Fiorentina | 2.48 | 3.30 | 2.75 |
| 20:45 | 2502 | Trabzonspor vs FC Basel | 1.85 | 3.70 | 3.85 |
| 20:45 | 3195 | Ajax vs Union Berlin | 1.94 | 3.45 | 3.79 |
| 20:45 | 3541 | Karabakh vs KAA Gent | 2.11 | 3.35 | 3.35 |
| 21:00 | 2096 | AF Amadou Diallo vs Bassam | 1.83 | 2.96 | 4.67 |
| 23:00 | 2204 | Sheriff Tiraspol vs Partizan | 2.69 | 3.14 | 2.64 |
| 23:00 | 3086 | AEK Larnaca vs SC Dnipro 1 | 2.06 | 3.30 | 3.55 |
| 23:00 | 3305 | Lazio vs CFR Cluj | 1.37 | 4.62 | 8.24 |
| 23:00 | 3309 | Sporting Lisbon vs Midtjylland | 1.33 | 5.18 | 8.17 |
| 23:00 | 3557 | Sevilla FC vs PSV Eindhoven | 2.21 | 3.35 | 3.15 |
| 23:00 | 4210 | Juventus vs Nantes | 1.42 | 4.37 | 7.43 |
| 23:00 | 4845 | Bayer Leverkusen vs Monaco | 1.95 | 3.64 | 3.55 |
| 23:00 | 5637 | Ludogorets Razgrad vs Anderlecht | 2.23 | 3.22 | 3.22 |
| 23:30 | 5102 | Cucuta Deportivo vs Once Caldas | 3.62 | 3.62 | 1.83 |

### IJUMAA - 17/02/2023

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1818 | Mirassol SP vs Ituano SP | 1.95 | 3.12 | 3.74 |
| 00:00 | 3658 | Japan W vs Brazil W | 2.75 | 3.32 | 2.29 |
| 00:00 | 4095 | Sebaco FC vs Deportivo Ocotal | 1.77 | 3.30 | 3.65 |
| 01:00 | 1093 | Atletico Catarinense SC vs Avai | 5.40 | 3.00 | 1.60 |
| 01:30 | 1871 | Santo Andre SP vs Santos | 3.32 | 3.16 | 2.07 |
| 01:30 | 4299 | Barranquilla FC vs Deportivo Cali | 2.64 | 3.42 | 2.33 |
| 02:30 | 3810 | Vasco da Gama vs Botafogo RJ | 2.68 | 2.94 | 2.58 |
| 02:30 | 4471 | Curico Unido vs Copiapo | 1.68 | 3.57 | 4.46 |
| 03:00 | 1182 | Zamora FC vs CA Boston River | 2.06 | 3.25 | 3.25 |
| 03:00 | 1197 | USA W vs Canada W | 1.74 | 3.53 | 4.10 |
| 03:30 | 5367 | Corinthians vs Palmeiras | 3.06 | 3.01 | 2.26 |
| 04:00 | 5132 | Atletico Nacional vs Deportivo Pereira | 1.63 | 3.57 | 4.87 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# YANGA, FEI TOTO

INATOKA UK. 24

kwenda Dubai kwa ajili ya mapumziko ya muda mfupi kabla ya kurejea nchini kusikiliza shauri lililokuwa linamkabili.

Mapema mwaka huu nyota huyo alionekana akifanya mazoezi na timu yake ya zamani ya JKU ambayo ilikuwa ikijiandaa na mashindano ya Kombe la Mapinduzi huko Visiwani Zanzibar.

Simba na Azam FC zilitajwa kumwinda Fei Toto, lakini mabosi wa timu hizo mbili walikanusha kuhusika na mchakato wa kumshawishi Mzanzibari huyo kuondoka katika klabu yake.

Viongozi mbalimbali wa serikali walitajwa kuhusika katika kumshawishi Fei Toto kurejea katika klabu hiyo na kwa nyakati tofauti mchezaji huyo alikaririwa akisema atakuwa tayari kucheza kwenye timu itakayomlipa maslahi mazuri.

Katika kuhakikisha anapata haki yake, Fei Toto alilazimika kuomba marejeo ya kesi yake ambayo ilifunguliwa na Yanga.

# MKUDE AKABIDHIWA MIKOBA

INATOKA UK. 24

Mama ametutuma na kuchagiza anataka tukawafunge Raja Casablanca, hiyo kazi Simba tunauweza wa kuifanya, tunaenda kupambana na kuchukua milioni 20, ninaimani atakuwa anaangalia mpira huo, basi Moses Phiri na wachezaji wengine ujumbe umewafikia," alisema Ahmed.

Alisema pia Simba inapokuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika michuano hiyo huwa ni kama timu iliyopo sayari nyingine kutokana na ubora wanaouonyesha. Mipango kuelekea mchezo huo iko vizuri na leo (jana) asubuhi, Saido Ntibazonkiza amerejea kikosini," alisema kiongozi huyo.

Pia amewataka mashabiki kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo ili kushuhudia watakavyowaopulizia 'pumzi' ya moto wapinzani wao, Raja Casablanca kama walivyofanya kwa timu nyingine walipocheza mechi hizo za kimataifa.

"Matokeo yote yaliyopatikana kwa Mkapa licha ya ubora wa benchi la ufundi na wachezaji wetu, mashabiki wamechagiza kwa asilimia kubwa. Silaha yetu kubwa ni mashabiki, wajitokeze kwa wingi kuwapa presha wapinzani wetu," aliongeza.

Alisema suala la jezi liko nje ya uwezo wao lakini alitoa shaka kwa kueleza zitawasili nchini kabla ya siku ya mchezo huo wa kwanza nyumbani.

# Michezo

Alhamisi Februari 16, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Mbappe atarajiwa kuibeba PSG Ulaya




Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu (kushoto) akipokea zawadi ya jezi kutoka kwa Mwenyekiti wa Tawi la Home Boys lililopo Wazo Hill, Dar es Salaam, Samweli Moshi 'Mgalilaya' (kulia), katika sherehe za uzinduzi wa kampeni ya kwenda kuujaza uwanja kuelekea mechi dhidi ya Raja Casablanca kutoka Morocco itakayochezwa keshokutwa. **PICHA: SIMBA SC**

# Yanga, Fei Toto mambo mazuri

●●●Ni baada ya kusaini mkataba mpya wa Sh. milioni 350 ili kurejea Jangwani na...

**Na Saada Akida**

HATIMAYE mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' wamemalizana na nyota huyo mwenye asili ya Zanzibar anatarajia kurejea katika kikosi cha timu hiyo hivi karibuni, imefahamika.

Fei Toto alitangaza kuvunja mkataba wake na Yanga kwa kuilipa kiasi cha Sh. milioni 112 lakini shauri hilo lilipopelekwa katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), iliamuru nyota huyo bado ni mchezaji wa klabu hiyo ya mitaa ya Jangwani na Twiga.

Lakini pia limeonekana kumalizika ikiwa zimepita siku chache tangu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, kuzitaka pande hizo mbili kukaa pamoja na kumaliza sintofahamu hiyo kwa kutumia busara.

Taarifa za uhakika zilizopatikana jijini Dar es Salaam kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wa Yanga walikwenda Zanzibar kufanya mazungumzo na mchezaji huyo na kufikia makubaliano mapya.

Chanzo chetu kilisema baada ya mazungumzo hayo, wamekubaliana kusaini mkataba mpya wa miaka miwili wenye thamani ya Sh. milioni 350 na atalipwa mshahara wa Sh. milioni 15 kwa mwezi.

"Ni kweli kulikuwa na mvutano mkubwa sana hadi sakata hili kufika katika ngazi ya juu hadi serikali kuingilia kati, hatimaye sakata limefikia mwisho baada ya busara kutumika kwa pande zote mbili," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza baada ya kukamilisha makubaliano hayo mapya, sasa Fei Toto anatarajia kuingia kambini baada ya Yanga kumaliza mchezo wake wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Imeelezwa Yanga imefikia uamuzi huo ili kuongeza nguvu katika kikosi chake kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia malengo ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA pamoja na kufika hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia gazeti hili nyota huyo anatakiwa kurejea katika majukumu ya klabu kwa ajili ya kulinda kipaji chake na manufaa kwa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

Nabi alisema Fei Toto ni mchezaji wa kutegemewa wa Yanga na Taifa Stars na kumalizika kwa sakata lake ni jambo la faraja.

Fei Toto amekuwa nje ya kikosi cha Yanga tangu Novemba mwaka jana na presha ya madai yake ya kuboresha mshahara wake ilishika kasi zaidi wakati dirisha dogo la usajili lilipofunguliwa.

Katika muda ambao hakuwa na kikosi cha Yanga, Fei Toto, alionekana ame-

INAENDELEA UK. 23

## Mkude akabidhiwa mikoba 'kuiua' Raja

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikikosa huduma ya kiungo, Sadio Kanoute, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', ametoa majukumu kwa nyota wake watatu kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca kutoka Morocco.

Kanoute atakosa huduma ya kiungo huyo kutokana na kuonyeshwa kadi tatu za njano na nafasi yake huenda ikachukuliwa na Ismael Sawadogo, Mzamiru Yassin, Jonas Mkude au Erasto Nyoni.

Tayari nyota hao wameanza kupewa majukumu kuelekea mchezo huo utakaochezwa keshokutwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Kanoute amekipa pengo kubwa kikosi chao na ambacho Robertinho alihitaji kuona kinafanya mashambulizi zaidi katika kusaka ushindi.

Ahmed alisema kocha anaamini pengo hilo litazibwa kikamilifu na Sawadogo, Mzamiru au Mkude ambaye hakuwa sehemu ya mipango ya mechi iliyopita na sasa yuko kambini kwa ajili ya kuwakabili Raja Casablanca.

"Mkude amejiunga kambini na anafanya mazoezi na wachezaji wenzake, suala la kucheza hilo litakuwa mipango ya benchi la ufundi, kulingana na mfumo anaotaka kuingia nao, ikiwa kutaka kushambulia sana, basi atawatumia Sawadogo na Mzamiru.

Hiyo itakuwa ni mipango ya kocha Robertinho, Mkude anafurahi ndani ya timu na yuko kambini, amepewa jukumu kubwa la 'kaka' kiongozi kwa wachezaji wenzake, hii ni baada ya kupitia changamoto nyingi za kupelekwa katika kamati ya nidhamu," alisema Ahmed.

Aliongeza mchezo wa Jumamosi utakuwa na jambo moja la kutafuta matokeo mazuri kwenye uwanja wa nyumbani na hawana jambo lingine tofauti na hilo na wachezaji wao wanatambua.

"Simba tunaamka siku hiyo kwa jambo moja kutafuta ushindi, licha ya kutaka pointi tatu lakini kutekeleza agizo la mama (Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa hamasa kwa wachezaji wetu kununua kila bao moja kwa Sh. milioni tano.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002